

**UCHANGANUZI WA KIISIMU WA BAADHI YA SEMI
KATIKA MATINI YA KIDINI: MTAZAMO WA
KIPRAGMATIKI**

NA

LYDIAH M. SHAVIYA

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya uzamili katika chuo kikuu cha Nairobi.

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine kile kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Sahihi _____ Tarehe _____

Lydia S. Mwenje

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi.

Sahihi _____ Tarehe _____

Prof. John Habwe

(Msimamizi)

Sahihi _____ Tarehe _____

Dkt. Hanah Mwaliwa

(Msimamizi)

TABARUKU

Ningependa kuitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa Robert Shaviya na Jenipher Nashimiyu kwa kuhakikisha kuwa nilipata msingi dhabiti wa masomo ambao uliniwezesha kufika kiwango hiki.

Ningependa kuitabaruku kazi hii kwa mume wangu mpendwa Benjamin Otieno na watoto wangu Hiram Jayvin na Hope Furaha ambao walifanya nitie bidi zaidi dhidi ya changamoto nyingi nilizokumbana nazo katika masomo yangu.

SHUKRANI

Ningependa kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na nguvu hadi nilipofanikiwa katika kazi hii.

Shukrani zangu za dhati ni kwa wasimamizi wangu Prof Habwe na Dkt Mwaliwa kwa kunielekeza bila kuchoka na kuhakikisha kuwa nimefaulu kupata shahada hii ya uzamili. Vilevile nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili kwa ushauri ulionielekeza katika kazi hii.

Namshukuru mume wangu ambaye tumetembea naye katika safari hii ya masomo; ulikuwa wa msaada mkubwa kwangu Mungu akubariki sana

Nawashukuru sana wanafunzi wenzangu wote ambao tulishirikiana katika mijadala tuliyokuwa nayo katika masomo haya na hata pia kutiana moyo mara kwa mara kulichangia zaidi katika ufanisi wangu.

Kuna wengine wengi ambao walinitia moyo kwa njia moja au nyingine mlinifaa sana na nimefanikiwa kwa sababu yenu Mungu awabariki sana.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
VIFUPISHO VYA MANENO.....	vii
IKISIRI	viii
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI	1
1.0 Usuli wa mada.....	1
1.1 Tatizo la utafiti.....	3
1.2 Madhumuni ya utafiti.....	4
1.3 Nadharia tete	5
1.4 Umuhimu wa utafiti	5
1.5 Upeo na mipaka ya utafiti	5
1.6 Misingi ya nadharia.....	6
1.6.1 Kubanika kwa neno.....	7
1.6.2 Kupanuka kwa neno.....	8
1.6.3 Kukisia kwa neno.....	9
1.7 Yaliyoandikwa kuhusiana na mada.....	10
1.8 Mbinu za utafiti.....	12
1.8.1 Njia za ukusanyaji data	12
1.8.2 Uchanganuzi wa data	13
1.9 Hitimisho.....	14
SURA YA PILI.....	15
LUGHA NA DINI	15
2.0 Utangulizi.....	15
2.1 Dhana ya lugha	15
2.2 Lugh na mawasiliiano	16
2.2.1 Lugh na muktadha	17
2.2.2 Muktadha wa kiisumu.....	17

2.2.3 Muktadha wa hali halisi	18
2.3 Lugha na mahubiri kanisani.....	18
2.4 Uhusiano wa lugha na dini.....	19
2.5 Dhana ya sajili.....	20
2.5.1 Sajili ya kidini	21
2.5.2 Sifa za sajili ya dini.....	22
2.6 Umuhimu wa matumizi ya baadhi ya semi katika matini ya kidini kipragmatiki.....	23
2.6.1 Ni njia ya kufunza kitu katika kiwango cha ndani	23
2.6.2 Kusababisha hali ya kujuu	24
2.6.3 Kuamsha hisia au kusisimua hisia	24
2.6.4 Kuvutia usikivu katika mazungumzo kwa msikilizaji	24
2.6.5 Kuwapawasikilizaji motisha ya kufanya jambo fulani.....	25
2.6.6 Hutumika kukiwa na ugumu wa kueleza kitu au hali fulani.....	25
2.6.7 Hutumika kwa kicheko au kufurahisha, kicheko chenyewe kinaweza kuwa cha	25
2.6.8 Ili kutumia maneno machache.....	25
2.6.9 Hutumika kwa sababu hakuna chaguo lingine la kueleza kile walichotaka kueleza.....	26
2.6.10 Kunukuu	26
2.6.11 Kuongeza utajiri kwenye mazungumzo	26
2.6.12 Kuyapa mazungumzo uhai	26
2.7 Hitimisho.....	27
SURA YA TATU	28
KUPANUKA NA KUKISIA KWA MAANA KWA SEMI KATIKA MAHUBIRI.....	28
3.0 Utangulizi.....	28
3.1 Wahubiri na matumizi ya lugha	29
3.2 Kupanuka kwa maana katika baadhi ya semi za kidini.....	30
3.3 Kukisia kwa maana kwa semi katika mahubiri.....	51
3.4 Kubanika kwa maana katika semi.....	53
3.5 Hitimisho.....	55
SURA YA NNE	56
4.0 Hitimisho.....	56
4.1 Maoni na mapendekezo	58
MAREJELEO	59

VIFUPISHO VYA MANENO

KBC Kenya Broadcasting Corporation

MBCI Ministry of the Body of Christ International

SAYARE Sauti ya Rehema

IKISIRI

Lengo kuu katika utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya lugha katika mahubiri ya kidini ya Kiswahili. Tasnifu hii inahusu uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya semi katika mahubiri ya kidini ya Kiswahili katika mtazamo wa kipragmatiki. Katika utafiti huu tulijikita katika mahubiri ya kipentekoste tuliyorekodi kutoka katika vituo vyta runinga vitatu teule ambavyo ni KBC, SAYARE na MBCI. Tuliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika ambayo inachunguza jinsi maana ya neno kiisimu inabadilika katika matumizi. Utafiti huu ulidhihirisha ya kuwa wahubiri wa kidini hutumia baadhi ya semi zenyet maana ya kiisimu ni tofauti na maana ya kimuktadha japo kwa viwango tofauti. Vilevile, muktadha wa matumizi ya baadhi ya semi katika mahubiri ya kidini ya Kiswahili huathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu. Pia ilidhihirika kuwa matumizi ya baadhi ya semi katika mahubiri ya kidini kipragmatiki yana umuhimu.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa mada

Lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano katika maisha ya mwanadamu. Mwanadamu huitumia lugha katika kufanikisha michakato ya kidini ikiwemo kusali na kutoa mahubiri. Lugha na dini ni vipengele ambavyo vina uhusiano mkubwa na haviwezi kutenganishwa. Kuna wataalamu mbalimbali ambao wamejadili kuhusu swala hili la lugha ya kidini.

Rahimi (2012) anasema mwingiliano kati ya lugha na dini umepuuzwa na wanaisimu nchini Iran ilihali vitengo hivi viwili vina uhusiano muhimu mionganoni mwa watu. Rahimi (2012) anaendelea kusema kuwa mazungumzo ya kawaida hayahitaji lugha maalum kama dini inavyohitaji, kwa sababu miktadha ya kidini na mazingira yake inahitaji maneno maalum. Juhudi za kujua na kuingiliana na ulimwengu mwingine zinahitaji matumizi ya hali ya juu ya rasilimali za kiisimu. Lugha ya kidini inatofautiana na lugha ya kawaida Kean (1997). Crystal (1969) anasema ili kujua zaidi kuhusu lugha, ni muhimu kuangalia muundo wa ndani na maana yake inayotegemea mzungumzaji. Crystal (1969) akimrejelea Malinowski anasema, haiwezekani kuelewa maneno katika lugha pasipokuwa kwa kiwango fulani kushiriki katika maisha sawa na mtumiaji.

Katika utafiti wa uhusiano wa lugha na dini, tafiti nyingi zimelenga lugha ya dini ya kikristo kwa ujumla ama matumizi ya lugha katika kanisa katoliki na vilevile matumizi ya lugha katika dini ya kiislamu. Hakujawa na utafiti ambao umeshughulikia uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya semi katika mahubiri ya kipentekoste katika msingi wa nadharia ya pragmatiki leksika.

Muktadha ni kipengele muhimu katika mawasiliano kwasababu maana hutokana na muktadha (Sharpe 2007). Wamitila (2008) anasema lugha hutofautiana kutegemea baadhi ya mazingira na muktadha inakotumiwa lugha hiyo. Kwa hivyo muktadha huchangia katika kuelewa maana ya maneno yanavyotumika katika lugha mbalimbali na kila lugha ina sifa zake zinazoitambulisha.

Dini ya kikristo ni kubwa sana ulimwenguni yenyewe wafuasi bilioni 2.4 ulimwenguni. BBC (2009) Ukristo uliibuka kutokana na uyahudi katika karne ya kwanza. Ukristo huu ultokana na mafunzo ya uhai, kifo na ufufuko wa Yesu Kristo. Wale wanaomfuata wanaitwa wakristo.

Ukristo una matawi mengi tofauti yanayotokana na imani na desturi tofauti. Matawi haya ni Ukatoliki, Orthodox ya mashariki na Uprotestanti. Kutoptokana na matawi haya makuu kuna matawi mengine madogo katika kila tawi. Kanisa la kipentekoste lilitokana na tawi kuu la uprotestanti.

Kwa mujibu wa Nthamburi (2015) imerekodiwa kuwa ukristo nchini Kenya ulianza miaka ya 1497, wakati ambapo Vasco da Gama alizuru nchi ya Kenya. Kanisa la kwanza lilirekodiwa miaka ya 1500, baadaye mwaka wa 1624, kukawa na vituo 54 vya mjini Mombasa. Kanisa la kwanza mjini pwani lilikuwa kanisa Katoliki, ambalo lilioka kwa kasi wakati wa karne ya 20 kwa sababu ya wakoloni.

Kanisa la kwanza lilikuwa Katoliki lakini kukawa na mabadiko yaliyoibua migawanyiko. Baada ya migawanyiko kukawa na kanisa la Katoliki ikiwasilishwa na asilimia ya 23.3%, kanisa la uprotestanti likiwakilishwa na 47.4% na wale ambao si wakatoliki waliwakilisha na asilimia 11.8%. Asilimia 17.5% ya idadi iliyosalia ya wakenya ilijumuisha dini zingine kama Dini ya kiislamu, Dini ya kihindi, Dini ya Bahai na dini nyinginezo. Kutoptokana na asilimia 47.4% ya waprotestanti, asilimia 70% inajumuisha makanisa ya kipentekoste. Kutoptokana na data hii ni wazi kuwa idadi ya wapentekoste ni kubwa. Takwimu hizi ni kwa mujibu wa Kenya Advisor (2015). Upentekoste ni sehemu ni sehemu ya ukristo inayokua kwa haraka ulimwenguni ikifuata ukatoliki kulingana na watafi kwa mujibu wa Jimfeen (2004).

Kanisa la kipentekoste lina upekee wake jinsi wanavyoabudu na kuendesha shughuli zake. Hili ni kanisa lakisasa na lenye mabadiliko na sifa za kipekee zinazolitofautisha na makanisa mengine ya kiprotestanti. Wapentekoste wanaamini katika kuokoka kwa kibinafsi kunakodhihirishwa kupitia kwa kujazwa na Roho Mtakatifu na kuongea kwa ndimi. Ibada zao huwa zenye haiba kubwa na mihemko inayoambatana na kupiga makofi, miziki ya kisasa na kucheza. Wahubiri wake huhubiri kwa nguvu na misisimko na mahubiri yao hupokelewa kwa furaha, kusimama, kuinua mikono na kupiga kelele. Pia wanaamini katika maono, ndoto, ishara, uponyaji na unabii. Kwa mujibu wa Lien-Yuehwei (2015) watu wasio wa kipentekoste huchukulia kuwa hayo ni matukio maalum ya kidini au vipawa vya kibinafsi vya kanisa hilo ambavyo havina maana ya kijumla katika makanisa mengine. Kanisa la kipentekoste lina lugha ya kiungu ya kiishara ambayo maana yake haiwezi kuelewaka kiakili na kwa maana ya

nje. Katika utafiti huu tulichunguza kipragmatiki matumizi ya lugha katika baadhi ya semi katika matini ya kidinikatika mahubiri ya Kiswahili.

Maneno katika mahubiri ya kidini hufasiriwa kwa njia ya kipekee, ambapo maana yake kimatumizi huwa tofauti na maana ya kiisimu. Kwa mfano, katika Bibilia, kitabu cha Yohana 10:18 kinasema, “Wote walionitangulia ni wevi na wanyang’anyi lakini kondoo hawakuwasikia.” Kwa mfano, neno kondoo lililotumiwa katika Bibilia katika lugha ya kawaida linamaanisha mnyama na pia mtu mpumbavu. Katika muktadha wa dini ya kikristo, neno hilo linamaanisha wafuasi au washirika katika kanisa. Watu amba si wa dini ya kikristo huenda wasifasiri neno hili kwa njia inayokusudiwa.

1.1 Tatizo la utafiti

Dini ni kiungo muhimu kwa binadamu wengi duniani. Ni muhimu kuzingatia namna ambavyo lugha inatumika katika dini kwa sababu kila dini ina upekee wake katika matumizi ya lugha. King’ei (1992) anasema lugha ya kidini huathiriwa sana na utamaduni ulioizaa ile dini. Kwa hivyo kila dini ina utamaduni wake unaoifanya kuwa ya kipekee katika kuendeleza shughuli zake. Katika matumizi ya lugha yoyote ile, ni muhimu kuzingatia jamii-lugha yake ili kufanikisha mawasiliano. Crystal (1969) amedai kuwa mzungumzaji hawezi kutumia mtindo mmoja wa mazungumzo anapozungumza na makundi tofauti ya watu. Anaendelea kusema kuwa, mzungumzaji akitaka kutoa ujumbe huzingatia mambo muhimu kama mada ya ujumbe, aina ya hadhira na mahitaji ya hadhira.

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuhusu matumizi ya lugha katika dini ya kikristo. Indede (2007) ameshughulikia sitiari na tashbih katika dini ya kikristo akiongozwa na nadharia ya umaanisho ya Grice. Katika utafiti wakeamelenga dini ya kikristu kwa ujumla. Waweru (2012), ameshughulikia ubadilishaji msimbo katika kanisa la katoliki akitumia nadharia ya umaanisho ya Grice (1975). Katika utafiti wake alilenga majimbo manne makuu tofauti nchini Kenya. Nthenya (2012) naye kwa upande mwagine ameangalia mikakati ya mawasiliano wanayotumia wakalimani katika makanisa teule ya kipentekoste ya Machakos nchini Kenya.

Uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya semi katika matini ya dini ya kipentekoste kwa msingi wa nadharia ya pragmatiki leksika haujashughulikiwa katika utafiti wowote kwa kiasi cha kuridhisha. Utafiti huu unadhamiria kuziba pengo hili. Pragmatiki leksika inahusiana na maana ya neno katika muktadha wa kimatumizi ambao huathiri maana ya neno hilo kiisimu. Katika kurejelea maana,hiki ni kipengele muhimu katika mawasiliano. Mawasiliano yoyote yale huwa ya kimuktadha kwa sababu huwa yanatokea katika hali fulani ambayo huathiri jinsi watu wanavyowasiliana kwa kutumia lugha. King`ei (1995) anasema kuwa, mawasiliano ya kweli hutokea tu pale ujumbe unapofasirika kwa njia ya usahihi na kwa maana ambayo mtungaji alikusudia. Haya yanategemea tu muktadha wa mawasiliano.

Ufasiri wa maneno katika muktadha wa kidini ni tofauti na ufasiri wa maneno hayo kiisimu.Wahubiri wa kidini, haswa wanaohubiri kupitia televisheni wanalenga hadhira ambayo ina watu wa kidini na wasio wa kidini. Katika matumizi ya baadhi ya semi kwenye mahubiri hayo, huenda yazuie au yafanikishe mawasiliano. Katika uhakiki wa matini ya kidini ya kipentekoste, baadhi ya maswali tuliyoyajibu nije, kuna semi gani zimetumika zenyemaana zake kimuktadha zinatofautiana na maana kiisimu? Je wasikilizaji wa kidini na wasio wa kidini watafasiri maneno hayo kwa njia sawa?

Nadharia ya pragmatiki leksika inasababisha ufasiri mpana wa maana za semi kutegemea muktadha zinamotumika.Ndio maana katika utafiti huu tukiongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika, tulichunguza jinsi muktadha wa matumizi wa baadhi ya semi katika matini ya kidini ya Kiswahili yanavyoathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu. Vilevile tulitambuasemi zenyе maana ya kiiisimu ni tofauti na maana ya kimuktadha zilizojitokeza katika mahubiri hayo na sababu za matumizi yake kipragmatiki.

1.2 Madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya kimsingi katika utafiti huu ni kwa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika kufanya uchanganuzi wa semi zilizotumika katika mahubiri ya kidini ya Kiswahili. Katika kufanikisha uchunguzi huu, tulishughulikia madhumuni yafuatayo:

1. Kubainisha semi zitakazojitokeza katika mahubiri ya kidini ya Kiswahili zenyе maana ya kiisimu ni tofauti na maana ya kimuktadha.
2. Kuonyesha jinsi muktadha wa matumizi ya baadhi ya semi katika matini ya kidini ya Kiswahili unavyoathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu.
3. Kutambua umuhimu wa matumizi ya baadhi ya semi katika matini ya kidini kipragmatiki.

1.3 Nadharia tete

1. Mahubiri ya kidini huwa na semi zenyе maana ya kiisimu ni tofauti na maana ya kimuktadha..
2. Muktadha wa matumizi ya baadhi ya semi katika mahubiri ya kidini ya kiswahili huathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu.
3. Matumizi ya baadhi ya semi kaika matini ya kidini kipragmatiki yana umuhimu.

1.4 Umuhimu wa utafiti

Matokeo ya utafiti huu yana umuhimu kwa sababu yanaonyesha uwezo wa nadharia ya pragmatiki leksika katika kuchambua baadhi ya semi katika matini ya kidini. Sababu kuu ya utafiti huu ni ya kiusomi. Utafiti huu ni tofauti na tafiti zingine ambazo zimewahi kufanywa. Hakujawahi kuwa na utafiti kuhusu uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya matini ya kidini ya Kiswahili. Utafiti huu tuliofanya utawafaa watafiti wengine ambao watafanya utafiti katika sajili ya kidini. Kutohana na utafiti huu wataweza kujua ni sehemu gani watatafiti vilevile kupata maarifa au kuongeza maarifa zaidi katika uwanja kiusomi.

1.5 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika na ulilenga dini ya kikristo ukijikita katika makanisa ya kipentekoste. Mahubiri ya kipentekoste huwasilishwa katika shughuli mbalimbali kwa mfano kwenye warsha za makanisa ya kipentekoste, shughuli za maziko na harusini. Utafiti huu ulijikita kwenye mahubiri ya kanisani.

Mahubiri hayo huwasilishwa kupitia njia mbalimbali kama kupitia kwa redio, televisheni na kupitia hata kwa mtandao. Katika utafiti huu tulijikita katika mahubiri ya Kiswahili ya kipentekoste yanayowasilishwa kupitia kwa vituo vya televisheni teule vya kitaifa nchini kenya. Tulichagua mahubiri ya Kiswahili ya kipentekoste na yanayowasilishwa kupitia kwa vituo vya televisheni vya KBC, MBCI na SAYARE. Tulirekodi tu vipindi teule vya mahubiri ya kipentekoste yaliyopeperushwa tu katika lugha ya Kiswahili. Lugha na dini ni maswala mapana na changamano. Kwa hivyo kwa sababu ya muda na upungufu wa kifedha tulijikita katika dini ya kikristo ambapo tulichanganua kipragmatiki baadhi ya maneno yaliyotumika katika mahubiri hayo.

1.6 Misingi ya nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika, iliyopendekezwa na kukuzwa na Blutner miaka ya 1990. Nadharia hii inachunguza jinsi maana ya neno kiisimu inabadilishwa katika matumizi. Katika nadharia hii maneno yanahakikiwa katika utaratibu fulani na kufasiriwa kulingana na muktadha fulani maalum wa matumizi. Kwa hivyo nadharia ya pragmatiki leksika imeundwa na semantiki leksika na pragmatiki leksika ambazo zote hushughulikia maana ya semi. Semantiki leksika inachunguza uhusiano kati ya neno na dhana inayosimbwa ilhali pragmatiki leksika inaeleza kwa nini wazo liliwasilishwa kwa kutumia neno linatofautiana na dhana iliyosimbwa.

Blutner (2011) anadai kuwa wazo la kimsingi kuhusu pragmatiki leksika ilianzishwa na McCawley (1978). McCawley akiguzia kanuni za mazungumzo za Grice (1967), alionyesha kuwa tofauti kati ya muundo wa isimu wa maana iliyosimbwa na fasiri iliyopendekezwa ni matokeo ya kanuni za kijumla za tabia za ushirikiano na huenda hatua kwa hatua zinazotabirika.

Blutner (2001) akiwarejelea Katz na Fodor (1963) wanasesma maana ya neno inategemea mandhari ya sentensi hiyo. Kulingana na Katz na Fodor (1963) mandhari yanahu habari za awali, mambo ya kijamii na maarifa ya kiisimu. Wanasisitiza kuwa maana kamilifu ya neno inapasa kuhusisha habari zaidi inayomwezesha mtu kupambanua maana ya maneno tofauti.

Kulingana na Blutner (2011), mambo ya kimsingi yanayoshughulikiwa katika pragmatiki leksika kulingana na Wilson (2003) na Cartson (2002), yanaweza kugawika katika mambo matatu ya kimsingi yafuatayo:

1. Kubanika kwa neno
2. Kukisia kwa neno
3. Upanuzi wa neno

1.6.1 Kubanika kwa neno


Hii ni hali ambapo neno linatumika kueleza maana finyu kuliko maana iliyosimbwa kisemantiki. Hiyo maana finyu ni lazima iwe inahusiana na muktadha wa matumizi ya neno hilo. Kwa mujibu wa Wilson (2006-7), kuna mfano, ‘Madaktari wote hunywa.’ Kitendo cha kunywa kina maana pana. Kitendo hiki kina maana ya kuweka mdomoni vitu kama chai, soda, maji ambavyo vinaweza kumiminika na kuvimeza. Katika muktadha huu ufasiri wa maana ya kunywa unajibana katika kunywa pombe na kufungia maana nyinginezo kama kunyua chai au maji.

Kwa mfano, katika muktadha wa kanisa la kipentekoste, Mhubiri anapohubiri anasema kuwa, ‘*Bwana anawapenda*’. Kulingana na maana ya kiisimu, neno *bwana* linamaanisha mume, mfalme au mtu mwenye cheo kubwa katika kazi fulani. Katika muktadha wa kanisa la kipentekoste, neno hili linamaanisha Mwenyezi *Mungu*. Kwa hivyo maana zingine zote za bwana zinafungiwa nje katika muktadha huo na kisha kuchukuwa ufasiri wa Mungu kama bwana anayerejelewa.

Okuku (2010) alitumia mfano kutokana na neno ‘*kuugua*’ambapo anasema kuwa maana ya neno hili ni ya kawaida tunavyojua kumaanisha kuwa mgonjwa. Akirejelea jamii ya wasamia anasema ukisikia mtu anasema kuwa ni mgonjwa, hasa akiwa na umri wa makamo, usemi huu utafasiriwa na msikilizaji kuwa mhusika anaugua ukimwi. Kwa hivyo hali ya ubanifu inafungia nje maana nyingine yoyote na kuruhusu ufasiri mmoja wa kuugua ukimwi.

Kubanika kwa maana wakati mwengine ufasiri wa neno fulani huwa unategemea kiasi au kiwango ambacho hali hiyo imetokea. Kwa mfano tukitumia neno ‘kunywa, mtu anapofasiri neno hili kwa kutegemea kiasi cha unywaji ambao anazungumzia. Kwa mfano mtu anaweza

kumuambia mwenzake, *Musa amekunywa leo* Kutohana na mfano huu, sentensi hii inamaanisha kuwa Musa amekunywa kupindukia.



1.6.2 Kupanuka kwa neno


Katika hali hii, neno lenye maana finyu linatumika kutoa maana ya kijumla. Yaani maana hupanuliwa zaidi kuliko ilivyo katika kategoria ya kisio. Blutner (2011) akimrejelea Sweetser (1990), anayetoa mifano ya maneno ya kiutambuzi akirejelea kitenzi *ona*. Neno *ona* lina maana ya kutumia macho ili kutazama kitu. Kwa mfano, “***Ona maji yale.***” Ni kumaanisha kutazama kwa macho au kutambua kwa macho.

Neno hilo pia linaweza kutumika kimuktadha kumaanisha picha anayokuwa nayo mtu katika akili yake. Kwa mfano, “*Niliona ulikokuwa ukielekea.*” Kumaanisha alijua alichotaka kufanya au kusema. Kwa hivyo, neno *ona* lenye maana finyu ya kutazama kwa kutumia macho, pia linaweza kutumika kutoa maana nyingine kimuktadha kuhusu picha anayokuwa nayo mtu akilini kwa hivyo nafasi ya ufasiri wa maana hupanuliwa zaidi. Sweetser (1990) anaeleza mambo kama haya yanahusiana na mpangilio wa kiakili.

Wamitila (2008) anasema hali ya upanuzi wa kimaana hutokea pale ambapo neno linapanuliwa kimaana, maana mahsus ya neno inapanuliwa na kuwa maana ya kijumla. Anaendelea kusema kuwa upanuzi huu unaweza kuchochewa na mazingira ya matumizi ya lugha-yawe ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kisaikolojia. Mfano ni neno ‘kupe ambalo zamani lilikuwa na maana ya mdudu anayenyonya damu lakini likapanuliwa kimaana kujumlisha ‘mnyonyaji anayetegemea jasho la wengine.

Oiro (2014) akiwarejelea Hock na Joseph (1996) ambao wanasema kuwa, njia moja kuu ambayo kwayo maneno hupata maana mpya na pana zaidi ni kwa matumizi ya sitiari. Kwa mfano maana


iliyosimbwa ya neno ‘Sungura’ ambaye ni mnyama mdogo lakini mwenye ujeuri mwingi. Tukilitumia neno hilo katika usemi kwa mfano; Juma ni Sungura. Maana ya usemi huu ni kuwa Juma ambaye ni mtu labda mdogo kama Sungura na ni mwenye ujanja



1.6.3 Kukisia kwa neno

Hii ni hali ya ufasiri ambapo neno lenye maana finyu linapanuliwa kimaana ili kuhusisha maana ya kitu kinachohusiana nacho ambacho kina maana tofauti na maana halisi ya neno hilo kiisimu. Jambo hili linajitokeza zaidi katika matumizi legevu kuhusiana na nambari au idadi. Kwa mfano Maria ambaye anahudhuria mkutano wa biashara na kisha anaulizwa kuwa ni watu wangapi ambao walihudhuria mkutano huo kisha aseme; *Watu elfu moja walihudhuria mkutano* ’Jibu hili katika muktadha wa matumizi halikumaanisha walikuwa elfu moja bali karibu watu elfu moja.

Mtu aliyehudhuria mkutano wa injili, alipoulizwa kuhusu idadi ya watu waliokoka katika mkutano huo alisema; *Maelfu na maelfu ya watu waliokoka katika mkutano wa injili* kumaanisha kuwa watu wengi sana waliokoka katika mkutano huo wa injili.



Nadharia hii ilituelekeza kubainisha maana ya kiisimu yabaadhi ya semi katika matini ya kidini ya Kiswahili zilizotumiwa katika mahubiri, kuhusiana na maana ya semi hizo katika muktadha

wa kidini wa kipentekoste. Katika kubainisha maana ya kiisimu na maana ya kimatumizi katika muktadha huo, tulichanganua matumizi ya semi hizo kwa kuzingatia maana tatu za kimsingi zinazojitokeza katika nadharia ya pragmatiki leksika. Maana hizo tatu ni kubanika, kukisia na kupanuka kwa maana. Kwa hivyo nadharia hii ilitufaa katika uhakiki semi katika matini ya kidini kipragmatiki katika mahubiri ya kipentekoste.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusiana na mada

Katika kusoma kwetu, tulipata tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa zinazokaribiana na kuhusiana na utafiti huu. Kuna tafiti ambazo zimeshughulikia dini mbalimbali na tamathali mbalimbali za usemi katika makala tofauti yaliyoongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika. Hakuna utafiti ambao unafanana na utafiti huu, lakini kazi hizo zilitufaa katika marejeleo.

Indede (2007) anaangalia lugha ya kitamathali katika mahubiri ya dini ya kikristu. Katika utafiti wake amejikita katika sitiari na tashbihi akiongozwa na nadharia ya umaanisho ya Grice. Utafiti wake umelenga makanisa ya kikristu kwa ujumla. Utafiti huu ni tofauti kwa sababu sisi tulifanya uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya semi katika matini ya kidini tukiongozwa na nadharia ya Blutner ya pragmatiki leksika.

Okombo (2011) amefanya uhakiki wa kintendo wa sitiari, taashira na tashbiha katika Utenzi wa dini ya Kiislamu wa Tambuka. Katika utafiti wake ameshughulikia dhana na aina za tamathali hizi za usemi pamoja na umuhimu wake. Utafiti huu unatofautiana kidogo na utafiti wetu kwa sababu sisi tulishughulikia uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya semi katika matini ya dini ya kikristo katika mtazamo wa kipragmatiki.

Mutiso (1996) ameshughulikia umboasili la motifu katika shairi la kiislamu la Kasida Ya Burudai. Katika shairi la Kasida Ya Burudai, Mutiso (1996) ameshughulikia ishara na uashiriaji mbalimbali unaopatikana katika shairi hilo katika dini ya kiislamu. Baadhi ya ishara alizoshughulikia ni kama simba, ndege, farasi, ngamia, mbuzi na kondoo. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu sisi tulifanya uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya semi katika matini ya dini ya kikristo.

Nthenya (2012) anaangalia mikakati ya mawasiliano wanayotumia wakalimani. Katika utafiti wake amelenga makanisa teule ya kipentekoste katika mji wa Machakos nchini Kenya. Katika

utafiti wake, Nthenya (2012) anachunguza ukalimani kutoka lugha ya Kingereza hadi lugha ya Kikamba. Nthenya (2012) anachunguza jinsi mkalimani anaweza aidha kufanikisha au kuzuia mawasiliano. Utafiti wake utatufaa kwa sababu utatusaidia kujua jinsi ya kufanikisha mawasiliano katika mahubiri ya kipentekoste. Utafiti wake ni tofauti na utafiti huu kwa sababu, sisi tuliangazia jinsi ufasiri wa baadhi ya semi katika mahubiri ya dini ya kikristo yanaweza kuzuia au kufanikisha mawasiliano kaika mahubiri.

Okuku (2010) anaangalia uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya matini za Kiswahili akitumia mtazamo wa pragmatiki leksika. Katika kazi yake ameshughulikia tamathali za semi akirejelea riwaya ya Kiswahili. Kazi yake ilitufaa katika utafiti huu kwa kuelewa nadharia ya pragmatiki leksika na matumizi yake. Utafiti wetu ni tofauti kwa sababu tuliangazia uchanganuzi wa kiisimu wa matini ya kidini.

Waweru (2012) ameshughulikia ubadilishanaji msimbo katika kanisa katoliki akiongozwa na nadharia ya umaanisho ya Grice (1975). Utafiti wake ulitufaa katika kuelewa uhusiano wa lugha na dini kwa ujumla. Utafiti wetu ni tofauti kwa sababu tulishughulikia uhakiki wa kipragmatiki wa matini ya kidini kwa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika.

Maana ya maneno katika lugha yoyote ile hutegemea muktadha uliotumiwa. Hii inaathiri uchaguzi wa maneno yanayotumiwa katika sentensi kama maana inayonuiwa na mzungumzaji inapaswa kuwa sawa na ya msikilizaji. Uchaguzi wa maneno unakuwa muhimu sana hasa unaposhughulikia masuala ya kidini.

Mambo haya yanaangaziwa kindani na Kean (1997) anaposema kuwa juhudzi za kujua na kuingiliana na ulimwengu-mwingine zinahitaji matumizi ya hali ya juu ya rasilimali za kiisimu. Kean (1997) anaendelea kusema kuwa lugha ya kidini inatofautiana na mazungumzo ya kila siku. Kean (1997) anasema hali ya mazungumzo ya kidini inatofautiana na hali ya mazungumzo ya kila siku katika njia mbalimbali.

Katika matumizi ya lugha yoyote ile, ni muhimu kuzingatia jamii-lugha yake ili kuweza kufanikisha mawasiliano. Crystal (1969) anataja vipengele vitatu muhimu vya kuzingatiwa na mzungumzaji anapotoa ujumbe wake. Mambo aliyoyataja ni mada ya ujumbe, aina ya hadhira na mahitaji ya hadhira.

Crystal (1969) anasema kuwa mzungumzaji hawezi kutumia mtindo mmoja wa mazungumzo akizungumza na makundi tofauti ya watu. Mzungumzaji ni lazima aeewe mahitaji ya hadhira yake anapotumia lugha. Mambo anayozungumzia Crystal (1969) yalitufaa katika utafiti huu kwa sababu yanachangia ufasiri wa ujumbe na msikilizaji ambao unaathiri mawasiliano ambayo ilikuwa kiini cha utafiti huu.

Katika utafiti huu tulichunguza uchaguzi wa maneno yanayotumika katika mazungumzo yanavyoweza kuathiri mawasiliano. Kwenye huu utafiti, tulichunguza jinsi matumizi ya baadhi ya semi katika mahubiri ya Kiswahili ya kipentekoste yanaweza kuzuia au kufanikisha mawasiliano kupitia vyombo vya habari.

Tamathali za semi hazitumiki tu katika muktadha wa dini peke yake, bali pia katika mazungumzo ya kawaida ya kila siku. Matumizi ya tamathali za semi yanaweza kuathiri kuelewa hisia na hata kuchukiza kundi-jamii fulani. Haya yamethibitishwa kutokana na utafiti wa Wangui (2010) ambaye alitafiti kuhusu ubaguzi unavyojidhihirisha kupitia matumizi ya lugha ya kitamathali ya Kikuyu. Katika lugha hii, mzungumzaji anaweza kuonyesha ubaguzi kwa kutumia tamathali ya semi fulani badala ya nyininge.

Oiro (2014) ameshughulikia uchanganuzi wa chuku na sitiari katika tamthilia za Kifo Kisimani na Sumu Ya Bafe akichukua mtazamo wa pragmatiki leksika. Kazi yake ilitufaa katika uelewa mpana wa nadharia ya pragmatiki leksika katika tamathali za semi hasa katika sitiari.

1.8 Mbinu za utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani. Tulijikita katika kanisa la kipentekoste ili kuepukana na mbinu mbalimbali zinazoweza kutatiza uchanganuzi wa data. Tulitambua semi zilizotumika na kisha tukachanganua kwa njia ya maelezo.

1.8.1 Njia za ukusanyaji data

Ili kutimiza malengo ya utafiti huu, tulikusanya data ya utafiti kwa kutumia njia ya kurekodi mahubiri kutoka kwenye televisheni. Tulirekodi mahubirikutoka kwa vituo vya televisheni teule KBC, MBCI na SAYARE. Tulichagua vituo vya televisheni ambavyo wahubiri wake ni wa kipentekoste na wanahubiri katika lugha ya Kiswahili. Mahubiri yaliyorekodiwa ni ya muhimu

kwetu kwa sababu tulikuwa tunachunguza matumizi ya baadhi ya semi zilivyonumika katika lugha ya Kiswahili. Tuliyaandika mahubiri haya na tukatambua semi zenye maana yake kiisimu ni tofauti na maana yake kimuktasha kisha tukazitumia katika uchanganuzi wa data.

Tulichagua hii njia ya ukusanyaji data kwa sababu kupitia njia ya televisheni watu wengi wanafikiwa katika sehemu mbalimbali za nchi. Wanaosikiliza mahubiri haya vilevile ni watu wenye vyeo, tabaka, kabilia, dini, viwango mbalimbali vya masomo, wakristo na watu wasio wakristo.

Katika utafiti huu, tuliwalenga wahubiri wa kipentekoste wanaohubiri katika lugha ya Kiswahili katika televisheni. Walengwa wetu wengine ni wasikilizaji wa dini tofauti. Tutachunguza uwezo wa wasikilizaji wa kufasiri baada ya uchanganuzi, kutokana na matokeo ya uchanganuzi yanayoonyesha utofauti wa ufasiri wa baadhi ya maneno katika mahubiri hayo kiisimu na kipragmatiki.

Tulitumia sampuli lengwa katika utafiti huu. Sampuli yetu ilikuwa wahubiri wa Kiswahili wa kipentekoste wanaohubiri katika vituo vya televisheni za kitaifa za kenya. Tulichagua vituo vya KBC, MBCI na SAYARE. Tulichagua vituo hivi kwa sababu vina vipindi vya mahubiri ya Kiswahili. Sampuli yetu ilijumuisha jumla ya wahubiri watano tofauti. Hawa walifaa kuwakilisha wahubiri wa kipentekoste ambao wanahubiri kupitia televisheni katika lugha ya Kiswahili.

1.8.2 Uchanganuzi wa data

Baada ya kukusanya data yetu, tulisikiliza mahubiri hayo na kisha kuyanakili kwenye karatasi. Tulitambua baadhi ya semi ambazo maana yake ya kiisimu ni tofauti na maana ya kimatumizi katika mahubiri hayo. Tuliweka semi hizi katika kategoria zake kwa misingi ya nadharia ya pragmatiki leksika inayotuongoza katika huu utafiti. Katika nadharia hii, maana dhahiri za maneno kiisimu hubadilika katika usemi. Mabadiliko hayo yamewekwa katika kategoria tatu za kimsingi ambazo ni kubanika kwa maana kupanuka kwa maana na kukisia kwa maana.

Kwa hivyo kutokana na nadharia hii, tulionyesha maana dhahiri ya kiisimu na maana ya kimkutadha ya semi tulizokuwa tumetambua kutoka kwenye data. Baadaye tulichanganua data hiyo kulingana na kategoria za mabadiliko ya kimsingi ya nadharia hii.

Tulitumia takwimu kubaini utofauti wa maana ya kiisimu na maana ya kimuktadha ya semi zilizotumika. Kulingana na utofauti wa maana ya kiisimu na maana ya kimkutadha ulivyokuwa umejitokeza tulifanya uamuzi kulingana na tatizo na madhumuni ya utafiti.

1.9 Hitimisho

Katika sura hii tulianza kwa kueleza tatizo na madhumuni ya utafiti. Tumeorodhesha nadharia tete zinazotuongoza katika utafiti na kuonyesha upeo na mipaka ya kazi katika utafiti huu. Kisha tumeangazia mambo yaliyoshughulikiwa na wataalamu mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu na kujadili kuhusu nadharia inayotuongozakatika utafiti. Tumeitatisha sura hii kwa kuangalia mbinu za utafiti ambazo tumetumia kukusanya na kuchanganua data.

SURA YA PILI

LUGHA NA DINI

2.0 Utangulizi

Katika sura hii tutajadili dhana ya lugha na uhusiano wa lugha na mawasiliano, muktadha na mahubiri kanisani. Vilevile tutashughulikia dhana ya sajili tukijikita kwenye sajili ya dini ambamo utafiti huu unahusika na kisha kuangazia sifa za sajili ya dini. Mawazo haya katika sura hii ni kulingana na michango ya wataalamu mbalimbali wa lugha na isimujamii. Baadaye tutajadili kuhusu umuhimu wa matumizi ya semi katika mahubiri kipragmatiki.

2.1 Dhana ya lugha

Lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano. Kupitia kwa lugha wanadamu wanaweza kuingiliana na kuwasiliana katika maisha yao ya kila siku. Lugha humwezesha mwanadamu kuendesha na kutekeleza shughuli muhimu katika maisha yake kama siasa, dini, elimu na utamaduni. Hata hivyo lugha ni chombo cha kuwaunganisha watu kwani huwaleta wanadamu pamoja. Pasipo na lugha hakuwezi kuwa na mawasilano.

Buliba na wenzake (2006) wanasema kuwa, lugha ni chombo kitendaji ambacho humwezesha mwanadamu kufafanua utamaduni wake na mazingira yake. Katika matumizi ya lugha ni muhimu mzungumzaji kuelewa wanajamii anaozungumza nao kwa sababu hiyo itamsaidia jinsi ya kutumia lugha. Lugha inayotumika katika makundi tofauti ya jamii hutofautiana na ina sifa zake za kipekee. Nganje (2008) anasema kuwa lugha yatakiwa iwe fasaha na yenyewe uteuzi wa msamiati ufaao.

Mukhwana (1990) anasema kuwa lugha haiwezi kutenganishwa na jamii, maana mahusiano ya lugha ni mahusiano ya kijamii. Pia anaendelea kusema kuwa kuchagua lugha fulani itumike mahali fulani na watu fulani hufanywa ili kuathiri muundo wa jamii husika na kutosheleza mahitaji fulani ya kijamii. Hii ina maana kuwa jamii hutumia lugha fulani katika muktadha ambao unaruhusu aina hiyo ya lugha kutumika. Wazungumzaji hutumia aina fulani ya lugha kwa nia fulani.

Utafiti wetu unachunguza matini ya kidini ya kiswahili. Nafasi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya ni jambo la kimsingi kwa watumizi na matumizi ya lugha hii. Hii ndio lugha rasmi na lugha ya taifa. Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanasema taifa ni kikundi cha watu wanaojitambulisha na chimbuko au usuli mmoja. Lugha ya taifa ni lugha inayotumiwa na watu wa taifa fulani. Lugha hii hutumiwa kuwaunganisha watu wa taifa hilo. Ili lugha iweze kupewa hadhi ya kuwa lugha ya taifa huwa imevuka mipaka ya kikabila na inapaswa kutumiwa na watu wote kama njia ya kuwasawazisha. Kiswahili kama lugha ya taifa hutumiwa wakati wa maingiliano baina ya watu mbalimbali. Matumizi ya lugha ya kiswahili katika mahubiri hufikia idadi kubwa ya watu wa kila aina nchini Kenya.

2.2 Lugha na mawasiliano

Mawasiliano ni utaratibu wa kuhamisha ujumbe kutoka kwa mwasilishi hadi kwa mpokezi, kupidia matumizi ya lugha kwa mujibu wa Buliba na wenzake (2006). Wanaendelea kusema kuwa ujumbe unajumuisha taarifa, mawazo, hisia au mwelekeo wa mwasilishi kulingana na namna ambavyo anaelewana na mlengwa wa mawasiliano.

Mzungumzaji yejote yule anapoitumia lugha huwa na lengo la kuwasiliana kikamilifu na wazungumzaji wake. Yawe ni mazungumzo ya kisiasa, ya ofisi, soko na ya kidini. Kinge'i (1992) anasema kuwa, mawasiliano yanaweza kuwepo iwapo maneno yanayotumika ni yenye kueleweka barabara na wanaohusika. Anaendelea kusema kuwa, katika mawasiliano ya lugha ni lazima mwenye kuwasilisha ujumbe fulani, kuutoa ule ujumbe kwa njia ambayo anayewasilishiwa ateweza kuufasiri bila shida yoyote. Yule anayetuma ujumbe huwa na nia fulani ambayo hutarajia kuwa anayepokea ujumbe huo aupate hivyo. Mawasiliano hutokana na pande mbili, yaani mwenye kuwasilisha habari na msikilizaji kama ilivyo kwenye mchoro huu.

Mawasiliano ya njia moja



Katika mawasiliano kuna vipengele muhimu vya kuzingatia kama:

Mtungaji ujumbe

Ni mhusika anayesema ujumbe ambao analenga kuwasilisha pamoja na namna ambavyo analenga kumwathiri mpokezi.

Njia ya mawasiliano

Ni athari jumulifu ya msimbo, mtindo, mbinu na chombo anachotumia mwasilishi kwa minajili ya kufanikisha mawasiliano.

Mpokeaji ujumbe

Huyu ni mlenngwa wa ujumbe anavyojitambua mwenyewe na kutambulishwa na mwasilishi kupidia kigezo cha matumizi ya lugha.

Muktadha

Haya ni hali au mazingira ambamo mazungumzo yanatokea. Muktadha huathiri pakubwa maana ya semi inayotumika. Mawasiliano yoyote yale yanaweza kukamilika au yasikamilike kwa sababu ya mambo ambayo yanaweza kuzuia au kufanikisha mawasiliano hayo.

2.2.1 Lugha na muktadha

Muktadha wa tamko fulani unaathiri kwa kiasi kikubwa maana ya tamko lenyewe au jinsi litakavyofasiriwa. Muktadha huo unaweza kuwa wa kiusemaji au wa kutolea tamko lenyewe au wa kulipokea, yaani kuna muktadha asili na muktadha pokezi kulingana na Romany (2010) akimrejelea Wavriner na Francis (1977) ambapo wanataja aina mbili za miktadha ambazo nimuktadha wa kiisimu na muktadha halisi.

2.2.2 Muktadha wa kiisimu

Huu ni muktadha unaohusu matumizi ya matini au sentensi ambamo neno fulani limetumika. Akimrejelea Yule (2004), anaeleza kuwa muktadha wa kiisimu kuwa hudokeza maana za maneno kama inavyotokea katika muktadha wa maneno katika kipindi kimoja. Aliwaauliza

wanafunzi kutoa sentensi kubainisha maana tofauti za neno tupa ambapo alipata majibu yafuatayo:

- i. Mkulima alitumia tupa kunoa upanga wake.
- ii. Mtoto ametupa uchafu kwenye biwi.
- iii. Selemani amemtupa Sofia kwa sababu ya tabia zake mbaya.

Inadhihirika kuwa neno tupa likitumiwa pamoja na maneno mengine kama upanga na kisu au litumike pamoja na maneno mengine kama uchafu ama mapenzi inakuwa rahisi kukisia maana inayokusudiwa. Maana ya neno inapatikana kwa kulihusisha neno hilo na maneno yaliyotajwa.

2.2.3 Muktadha wa hali halisi

Muktadha huu hurejelea mazingira mahsusini ambamo neno fulani linatumwiwa. Inakuwa vigumu kwa mzungumzaji asiyekuwa katika mazingira hayo au kushiriki katika shughuli husika au na tajiriba fulani katika shughuli hiyo kuelewa maana iliyokusudiwa. Hali ya kimazingira inamaanisha kuwa ni lazima kushuhudia vitu au matendo katika hali halisi ili kung'amu maana za vitu na matendo hayo. Aina moja ya kimuktadha pekee haiwezi kutosheleza mahitaji ya ufundishaji wa msamiati. Itabidi aina zingine za kimuktadha zihuashwe.

Kwa hivyo Romany (2010) akimrejelea Rivers (1984) anapendekeza kuwa kuna msamiati unaohitaji kufundishwa katika mazingira maalum kama jikoni au kwenye karakana. Kwa kufanya hivyo, miktadha hiyo tofauti itachangia katika kuelewa msamiati.

Lugha inayotumika katika makundi tofauti ya jamii hutofautiana na ina sifa zake za kipekee. Lengo la matumizi yoyote ya lugha ile ni kukamilisha mawasiliano. Ili mawasiliano yaweze kukamilika, msikilizaji anapasa kufasiri ujumbe kwa njia inayokusudiwa na mzungumzaji. Haya yanategemea kama kuna uelewa wa muktadha wa mzunguzaji na msikilizaji.

2.3 Lugha na mahubiri kanisani

Kwenye mahubiri, inapasa mhubiri awasiliane kikamilifu na hadhira yake. Katika ujumbe ambao anawasilisha, mhubiri anapopitisha mahubiri yake kuitia kwa runinga, huwa anakusudia kuwa wasikilizaji wake wanapata ujumbe na kufasiri huo ujumbe anavyokusudia. Mambo haya yakinmilika, basi mhubiri atakuwa ametimiza lengo lake.

Ili mhubiri kutimiza lengo hili, cha muhimu ni kulingana vile mhubiri huyu anatumia lugha yake ili kuhakikisha kuwa wanaohubiriwa wanafuata na kupokea mahubiri hayo anavyokusudia. Inakuwa vizuri kuwa atilie maanani utaratibu na sheria za mahubiri kuonyesha upekee wa lugha unaostahili katika sajili ya dini. Wairimu (2014) akimrejelea Brown na wenzake (1963:150) wanasema kuwa matumizi mazuri ya lugha yanaweza kutofautisha mhubiri mmoja na mwingine. Kutokana na mawazo haya, kila mhubiri ana upekee wake katika matumizi ya lugha.

Katika mahubiri, mhubiri hutumia lugha kwa njia tofauti labda kwa njia ya wazi au isiyo wazi kutegemea malengo mbalimbali. Hali hii ina athari kwa wale wanaopokea ujumbe. Lugha ni chombo muhimu kama njia ya mawasiliano na dini inahitaji lugha pakubwa kwa sababu ndiyo njia ya kuwaleta pamoja mhubiri na hadhira yake. Uhusiano kati ya lugha na watumiaji wake hauwezi kutenganishwa.

2.4 Uhusiano wa lugha na dini

Dini ni asasi ambayo ni muhimu katika maisha ya mwanadamu kwa sababu inahusiana na wanadamu kwa njia ya moja kwa moja. Ouma (2013) akimrejelea Gatakaa (2013) anaeleza kuwa imani na nguvu zote za binadamu hutiwa kwenye dini na hasa kiumbe mwenye nguvu anayetegemewa na wafuasi wa dini hiyo. Kutokana na mawazo haya ni vigumu kutenganisha dini na maisha ya mwanadamu.

Lugha ya kidini inatofautiana na lugha ya mazungumzo ya kila siku, anasema Kean (1997). Inabainika wazi kuwa lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano cha mwanadamu. Pasipokuwa na lugha inakuwa vigumu wanadamu kuingiliana katika shughuli zao za kila siku.

Lugha ina uhusiano mkubwa na dini ambayo ni kiungo muhimu katika maisha ya binadamu na jamii kwa ujumla. Dini ni mwangaza na mwongozo katika maisha ya mwanadamu ambapo hutumika katika kutekeleza shughuli zake kama kutoa mahubiri, kusali na katika shughuli za mazishi. Kwa njia moja ama nyingine lugha huleta utangamano mkubwa katika jamii. Kulingana na Ugwueye na Ohaeto (2012), Kupata dini au kuingia kwenye dini mtu anahitaji kwa kiwango fulani msamiati na sintaksia mpya. Lugha na dini vinahusiana kwa njia ambayo huwaunganisha watumizi wake ambao huzungumza lugha moja. Watu wanaozungumza lugha moja wanaweza

kuwa na urafiki wa karibu kuliko wale ambao hawatumii lugha moja ya mawasiliano. Inaweza kuwa vigumu mtu kuelewa lugha ya dini kama hayuko kwenye dini hiyo.

2.5 Dhana ya sajili

Kila jamii lugha ina sifa zake zinazoitambulisha lugha inayotumiwa. Nganje (2008) anasema kuwa lugha hutofautiana kutegemea mazingira na matumizi. Mawazo haya yanamaanisha kuwa mtu hutumia lugha fulani kutegemea mahali alipo kwa mfano sokoni, ofisini shulenii na kanisani. Nganje (2008) anaendelea kueleza kuwa lugha hutofautiana kutegemea mazingira, matumizi na nyanja mbalimbali zina msamiati maalum unaojenga sajili.

Buliba na wengine (2006) wanasema sajili ni mtindo au namna mbalimbali za matumizi ya ile lugha moja. Lugha katika upekee wake hukosa kukidhi mahitaji ya wanaotumia katika nyanja zote za mawasiliano. Ni kutokana na hali hii ambapo makundi fulani ya wanaotumia lugha hutokea na namna mbalimbali za kutumia lugha ile moja.lugha hii huwa tofauti na lugha ya kawaida.Namna hizi za kutumia lugha ndizo zinazorejelewa kama sajili au rejestaa.

Iribemwangi na Mukhwana (2009:19) wanaeleza kuwa,sajili katika isimujamii humaanisha mikondo ya kimawasiliano itumiwayo katika hali na miktadha fulani maalum. Wanamuunga mkono Halliday kuhusu mambo yafuatayo yanayoathiri sajili:

- a) Utaratibu wa mahusiano ya maisha. Wanasema kuwa huu ni uhusiano baina ya mzungumzaji na mzungumziwa.
- b) Uwanja unaozungumziwa. Mada zinazozungumziwa na mahali zinakozungumziwa ni muhimu katika kufafanua sajili.
- c) Mtindo au namna. Wanasema kuwa hii ni jinsi ya kufanya jambo. Katika sajili, mtindo ni njia ya mawasiliano kwa mfano lugha iliyoandikwa au ya mazungumzo.

Wanaismu hawa wanasema kuwa, sajili hujitokeza wazi katika mazingira fulani mahsus. Kutokana na maelezo haya ni kumaanisha kuwa sajili huwa tofautikutegemea jamii lugha. Sajili hutofautiana kutokana na mambo kama shughuli, mada, jinsia,umri na matumizi ya lugha. Kutokana na maelezo haya ndio maana kuna aina mbalimbali za sajili za lugha kama:

sajili ya sheria, sajili ya biashara, sajili ya sayansi sajili ya polisi na sajili ya dini. Kila sajili ina upkee wake katika matumizi ya lugha. Wamitila (2008) amejadili sifa mbalimbali za sajili.

Sajili hufasiliwa kwa kuangalia ni kitu gani anachokifanya mzungumzaji au mtumiaji wa lugha na lugha inayohusika katika kipindi fulani maalum. Kitu ambacho mtu anafanya ni kurejelea shughuli ambayo mtu anajihuisha nayo kwa wakati fulani. Sajili hujitokeza kutegemea shughuli. Hata kama mahali ni pamoja, sajili itatofautiana kutegemea shughuli inayoendeshwa mahali hapo. Kwa mfano, lugha itumiwayo katika maeneo ya kuabudu si sawa kila wakati, sajili hii itatofautiana kama shughuli ya ibada ya harusi.

Pili, sajili huwa na ruwaza au mtindo fungo ya msamiati na sarufi ambayo huhuishwa na hupatikana katika muktadha fulani. Kila sajili huwa na msamiati wa aina fulani unaotokea kwa wingi. Kwa mfano, lugha ya wavuvi itajaa majina ya viumbe wa majini hasa samaki na vifaa vya uvuvi na vyombo vya usafiri majini.

Vilevile sajili huweza kubainishwa kwa urahisi kwa kuangalia sifa maalum ambazo huwa vitambulishi vya uwanja unaohusika. Kanuni zinazotawala matumizi ya lugha hutegemea sajili. Kwa mfano lugha ya kitaalamu huhitaji maneno yatamkwe kikamilifu na kwa usahihi. Msamiati unaotumiwa katika uwanja fulani unaweza kuunda ‘kikoa’ fulani ambacho huweza kuelezwu kwa urahisi.

Sajili hufungwa kwa muktadha. Muktadha ni mazingira ambamo mazungumzo yanafanyika. Yanaweza kuwa bungeni, mnadani, posta, benki, kiwandani na kwingineko. Mazingira haya huwafanya waliomo kuibua maneno maalum katika uwanja husika.

2.5.1Sajili ya kidini

Dini ni mahali waumini hukusanyika kua shughuli za kuabudu. Mahali pale panaweza kuwa kanisani, msikitini, hekaluni au mahali maalum palipotengwa kwa ajili ya kuabudu. Aidha shughuli za ibada zinaweza kutokea uwanjani au chini ya mti. Mahali popote ibada hutokea, lugha hutokea. Lugha inayotumika pale huwa ni lugha ya kipekee. Kila anayehusika, awe ni mhubiri, mwenye uzoefu au muumini wa kawaida, hubidi atumie lugha yenye sifa fulani na hutambulishwa kwa sifa hizo.

Kama tulivyojadili awali sajili ni matumizi ya lugha katika uwanja maalum. King'ei (1992) anasema ibada na dhana zote kuhusu Munguhuwa na mtindo maalum ambao mara kwa mara huwa ni tofauti sana na matumizi ya lugha ya kawaida na huwa ni vigumu kuelewaka na watu wasioulewa uwanja wa dini na muktadha wa matumizi. Anaendelea kusema kuwa matumizi ya lugha na msamiati katika uwanja wa kidini hubadilika kutokana na kubadilika kwa lugha inayohusika na lugha ya kidini huathiriwa na utamaduni ulioizaa ile dini. Vilevile Stockwell (2007:7) anasema kuwa sajili mbalimbali sharti zifungamanishwe na matarajio ya tamaduni. Kila utamaduni una matarajio yake kwa mfano tamaduni zinahitaji mtu kutumia lugha ya heshima hasa mbele ya hadhira. Buliba na wenzake (2006) wanasema msamiati wa kawaida unawakilisha maana za kidini zinazofasili uhusiano bora wa watu na Mungu au miungu kwa upande mmoja na uhusiano adilifu wa waumini wenyewe.

2.5.2 Sifa za sajili ya dini

Sajili ya dini hutumiwa na watu kueleza itikadi yao au imani yao. Popote ibada inapotokea, lugha huwa na sifa za kipekee. Kila anayehusika awe ni mhubiri mwenye uzoefu au muumini wa kawaida, hubidi atumie lugha yenyе sifa fulani na hutambulishwa kwa sifa maalum. Wanaisimu mbalimbali wakiwemo Mathooko (2007) na Chesebe (2011) walijadili sifa za sajili ya dini kama zifuatazo:

Ukale wa lugha

Kitambulisho kikubwa cha sajili hii ni matumizi ya maneno ya kale, hata katika ibada za kiasili, msamiati unaotumiwa ni ule uliopokezwa kizazi hadi kizazi. Msamiati huu hutumika ili kuhifadhi ujumbe kama ulivyotolewa katika maandishi au mawasiliano ya zamani. Aidha waumini huhisi kwamba mabadiliko ya lugha yatabadilisha ujumbe au kupotosha maana asilia. Kwa mfano, Abraham akamjua Sara wakapata mwana.

Msamiati maalum

Aghalabu lugha inayotumika maabadani ni ya wastani. Yaani msamiati unaoelewaka na watu wa kila kiwango cha maisha kwa sababu kanisani kunakuwa na watu wa kila aina na viwango mbalimbali.

Matumizi maalum ya lugha

Ni rahisi kutambua sajili ya maabadani kutokana na matumizi ya tamathali za usemi kama vile mafumbo, jazanda, taswira na istiari. Kwa mfano, simba wa Yuda, nyota, juu, mwezi na moto.

Matumizi masimulizi yenye vielelezo

Lugha hii hutumika hivi ili kuelimisha, kushawishi, kuamuru, kuasa na kuelekeza. Masimulizi haya wakati mwagine huwa yanatokea kutoka kwa vifungu wanavyonukuu kutoka kwenye vitabu vitakatifu kama Biblia.

Kuchanganya na kuhamisha msimbo

Mara nyingi, wahubiri na hata waumini hutumia msimbo tofauti. Wahubiri hubadilisha msimbo kwa sababu mbalimbali kama kusisitiza ujumbe, kunukuu ujumbe kutoka kwenye vitabu vitakatifu, na pia ni njia ya kujieleza kama mzungumzaji hana maneno yanayofaa katika lugha hiyo.

Kurejelea vifungu vya Bibilia: Ujumbe unaotolewa maabadani huandamana na vifungu fulani vya Bibilia na Kurani Takatifu ili kuthiiibitisha au kusisitiza yanayoelezwa.

Matumizi ya lugha yenye unyenyekevu: Wahubiri na waumini hujinyenyekeza kwa Mwenyezi Mungu katika ibada.

Kuchanganya mahubiri na nyimbo: Mahubiri huendelezwa pia kwa nyimbo na maombi katika ibada.

2.6 Umuhimu wa matumizi ya baadhi ya semi katika matini ya kidini kipragmatiki

Pragmatiki ni taaluma inayochunguza lugha kimatumizi. Ni uchunguzi wa usemi hasa maana ambayo msemaji analenga kuwasilisha kuititia usemi huo.

2.6.1 Ni njia ya kufunza kitu katika kiwango cha ndani [1]

Nimekimbia huku na kule nikitafuta pesa.

Mzungumzaji kusema alikuwa anakimbia huku na kule akitafuta pesa haimanishi kuwa alikuwa anakimbia kwa miguu yake kwa mwendo wa kasi akitafuta mahali pesa zilipo. Maana ya usemi huo ni kumaanisha kuwa alikuwa katika shughuli ya haraka ya kutafuta pesa ambazo huenda ilikuwa vigumu kupatikana.

[2]

Siwezi kujisaidia mwenyewe nimeshindwa.

Ni kumaanisha kuwa katika shughuli zako haujafanikiwa na hauoni dalili ya kufanikiwa.

2.6.2 Kusababisha hali ya kujua

Watu hupenda kutambua kitu na tusipotambua kitu ubongo wetu hujaribu iwezekenavyo kupata uelewa wa kile tunachotafuta. Katika matumizi ya sitiari akili inafanya kazi ya kutafuta na kutambua tunachotaka kujua.

2.6.3 Kuamsha hisia au kusisimua hisia

Katika matumizi ya baadhi ya semi hisia zetu huamka huenda ukawa na hisia fulani kwa mfano ikiwa ulikuwa umedhoofika unakuwa na nguvu.

[3]

Wewe ni mwangaza wetu.

Kama mtu anayeambiwa alikuwa na hisia duni, anakuwa na nguvu akijiamini kwa sababu wengine wanamuamini.

2.6.4 Kuvutia usikivu katika mazungumzo kwa msikilizaji

Semi kama sitiari zinapotumika katika mazungumzo huvutia usikivu au umakini kwa msikilizaji. Hali hii hutokea kutegemea aina ya sitiari.

[4]

Huyo jamaa ni Simba kweli.

Kwa sababu wanaosikiliza wanajua sifa za simba kuna maelezo zaidi watakayotarajia kufuata. Labda mtu huyo alifanya nini na matokeo yakawa namna gani.

2.6.5 Kuwapawasikilizaji motisha ya kufanya jambo fulani

Semi hizi huwapa wasikiliza mshawasha na kuwa katika hali ya kuchangamka kutekeleza kitu fulani.

[5]

Tuwe na bidii ya mchwa katika shughuli hii kwa sababu tuna jukumu kubwa kule mbele.

Tunavyojua mchwa hawapumziki hufanya bidii sana ilhali ni wadudu wadogo. Kwa hivyo wasikilizaji wanaangalia mchwa kisha wanajiona kuwa wanaweza kufanya bidii zaidi hata kuliko mchwa.

2.6.6 Hutumika kukiwa na ugumu wa kueleza kitu au hali fulani

Kwa hivyo tunakopa neno au kirai kinachoonekana sawa na kitu au hali unayoeleza.

[6]

Shughuli hiyo ni mawe

Matumizi ya sitiari ni vigumu kueleza wazi kuhusu shughuli hiyo labda kuna ugumu usiosemeka.

2.6.7 Hutumika kwa kicheko au kufurahisha, kicheko chenyewe kinaweza kuwa cha kudhihaki au dhara

[7]

Maria ni maembe.

2.6.8 Ili kutumia maneno machache

Matumizi ya semi huchukua maneno machache kuliko maelezo mengi yanayotumika katika maelezo.

2.6.9 Hutumika kwa sababu hakuna chaguo linge la kueleza kile walichotaka kueleza

Pia kile unachoeleza huenda kimetumika mara kwa mara kwa njia hiyo moja.

Tasfida

Baadhi ya semi hutumika kuficha ukali wa maneno mengine ambayo hayawezi kutamkwa mbele ya watu au kama matusi.

[8]

Juma ni mwanamke.

2.6.10 Kunukuu

Kuna semi ambazo hunukuliwa kutoka kwenye Biblia kuonyesha kuwa hayo hayakuwa maneno yake mwenyewe bali ni kutoka kwenye Biblia.

[9]

Mathayo 6:22

Taa ya mwili ni jicho; basi jicho hilo lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru

2.6.11 Kuongeza utajiri kwenye mazungumzo

Matumizi ya semi huongeza utajiri katoka mazungumzo na kuyafanya kuwa na uzito fulani hivyo kuupa maana isiyo ya kawaida.

2.6.12 Kuyapa mazungumzo uhai

Matumizi ya semi katika mazungumzo huyapa mazungumzo uhai hivyo wasikilizaji matumaini hasa mazungumzo ya kidini

[10]

Ukinywa maji ya uzima hutaona kiu tena.

Maji ya uzima kama ishara yanawapa wasikilizaji matumaini ya uhai na hali ya uridhisho kwa sababu maji ni ishara ya uhai na kupata hali ya kutosheka.

2.7 Hitimisho

Katika hii sura tumejadili dhana ya lugha na uhusiano wake na mawasiliano, muktadha, mahubiri kanisani na dini. Tumejadili dhana ya sajili ambapo tulishughulikia sifa bainifu za lugha ya kidini kwa ujumla na kujikita katika sajili ya kidini ambamo utafiti huu unahusika. Kisha tumeangazia sifa za sajili ya kidini kulingana na mawazo ya wanaisimu mbalimbali na baadaye tumetambua umuhimu wa matumizi ya baadhi ya semi katika matini ya kidini kipragmatiki.

SURA YA TATU
KUPANUKA NA KUKISIA KWA MAANA KWA SEMI KATIKA
MAHUBIRI

3.0 Utangulizi

Mhubiri katika mahubiri yake hulenga kuwafikia na kuwafaidi wasikilizaji wake kupidia kituo hicho cha runinga. Mahubiri yaliyowasilishwa kupidia kwa vituo tofauti vyta runinga kama KBC, yanawalenga wasikilizaji wote wa kila aina kwa sababu kituo hiki kinatazamiwa kote nchini. Wasikilizaji wake wanatofautiana kwa mfano, wanaweza kuwa wanatoka katika dini mbalimbali, madhehebu tofauti, umri tofauti na viwango tofauti vyta masomo. Matumizi ya baadhi yasemi kipragmatiki yanaweza kufanikisha au kuzuia mawasiliano kwa njia moja ama nyingine. Hii inategemea jinsi makundi hayo tofauti ya wasikilizaji yanavyozifasiri hizo semi zilivyotumika na mhubiri huyo. Maana ya maneno kiisimu inatofautiana na maana ya kimuktadha wa matumizi ya maneno hayo. Swali ni je wasikilizaji wote wanafasiri huo ujumbe kwa njia sawa inavyokusudiwa na mhubiri?

Hata hivyo katika kutumia aina mbalimbali za semi kipragmatiki, wahubiri hao walikuwa na sababu maalumu. Wahubiri wengi walitumia semi ili kueleza maana ya ndani ya ujumbe wao, kusisimua hisia za wasikilizaji, kueleza kitu au hali fulani ambayo ni ngumu kueleza na wengine walitumia semi kipragmatiki kwa sababu zilikuwa zimenukuliwa kutoka kwenye Biblia ambayo ni msingi wa mahubiri hayo. Imeedhihirika kuwa kuna baadhi ya wahubiri amba walitumia baadhi ya semi kipragmatiki katika mahubiri yao bilakukusudia.

Katika utafiti huu tulilenga wahubiri wanaohubiri katika vituo vyta runinga vitatu ambavyo ni KBC, SAYARE na MBCI. Wahubiri hawa ni wa kipentaekoste lakini ni wa kutoka makanisa tofauti ya kipentekoste. Tuliwachagua wahubiri hawa kwa sababu kuna wale amba ni maarufu na wamehubiri kupidia kwa televisheni kwa muda mrefu. Kwa mfano mhubiri Pius Muiru katika kituo cha televisheni cha KBC katika jiji kuu la Nairobi. Pia kuna James Ng'ang'a na Harrison Ng'ang'a wanaohubiri jijini Nairobi wanaohubiri katika vituo vyta KBC na MBCI.

Katika utafiti huu pia tulilenga wahubiri wengine amba si maskofu na pia si maarufu nchini lakini ni wa kipentekoste. Baadhi ya wahubiri hao ni mhubiri Eli Rop katika kituo cha SAYARE

na mhubiri William katika kituo cha runinga cha MBCI. Vituo hivi hupeperusha vipindi nya kikristo pekee, tofauti na kituo cha runinga cha KBC ambacho hupeperusha vipindi vingine visivyo nya kikristo. Hata hivyo wahubiri hawa wote wana imani moja ya kipintekoste.

3.1 Wahubiri na matumizi ya lugha

Lugha kama chombo muhimu cha mawasiliano hutekeleza jukumu lake na watumiaji wa lugha hiyo. Maneno ambayo yamesemwa vizuri kwa wakati unaofaa, mawazo na taswira kuundwa vizuri yanaweza kuwa na athari kubwa kwa wasikilizaji. Mara nyingi muundo wa lugha ya mahubiri hutokana na mazingira na hali iliopo. Lugha inapata maana na umuhimu wake kutokana na muktadha na hali kulingana na Hillis (1997).

Kulingana na Lawless (1988), makundi ya watu na tamaduni hukuza lugha maalum zinazoleweka tu na wanakikundi hicho. Lugha hii maalumu huchora mipaka kuwatenga na kuwaweka wanakikundi pamoja. Hivyo ndivyo ilivyo katika kanisa la kipentekoste ambapo wana lugha yao ambayo wamepata katika kanisa hilo na matumizi yake yanatokana na muktadha. Hakuna mwongozo wa maneno haya ya kipentekoste bali yanatokana na Biblia na yana maana maalumu kwa watu wanaoyatumia. Maneno hayo mengine ni ya ndani sana hivi kwamba huenda watu wasio wa kipentekoste wasielewe maana yake.

Lawless (1988) anaendelea kusema kuwa kuna maneno ambayo ufanuzi wake umetokana na kikundi hicho. Wakati mwengine yanatumika na makundi mengine ya kikristo lakini yana uzito fulani katika kanisa la kipentekoste. Maarifa ya lugha maalum ya kipentekoste yaliyotokana na utamaduni wa kipentekoste yanapitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwengine na kikundi kimoja na kingine katika kanisa na hata jamii. Ugot (2013) anasema kuwa lugha ya kanisa inapitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na imekuwa ikikua na kubadilika kwa sababu lugha ni elimumwendo.

Kila dini ina upekee wake kulingana na imani na utamaduni wake. Nthenya (2012) anasema kuwa wanajamii katika dini wanatarajiwa kushiriki katika matarajio ya jamii lugha. Kutokana na upekee wa kila dini pia lugha inayotumika hufasiriwa kwa njia ya kipekee. Hills (1997) anasema kuwa lugha inapata maana na makusudi yake kutokana na muktadha wa jamii. Kanisa la kipentekoste hufasiri ujumbe kwa njia yake ya kipekee.

Katika uchanganuzi wetu tuliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner. Kulingana na Blutner (2011), mambo ya kimsingi yanayoshughulikiwa katika pragmatiki leksika akiwarejelea Wilson (2003) na Cartson (2002) yanaweza kugawika katika mambo matatu ya kimsingi ambayo tiliyatumbia katika uchanganuzi. Maana hizi kuu ni;

1. Kubanika kwa maana
2. Kupanuka kwa maana
3. Kukisia kwa maana

3.2 Kupanuka kwa maana katika baadhi ya semi za kidini

Hii ni hali ambapo neno linalorejelea kitu kimoja katika hali ya kawaida linatumika kurejelea maana pana zaidi ya maana iliyosimbwa kisemantiki katika neno hilo. Kwa mfano, Yesu ni simba wa Yuda. Kutokana na mfano huu, sifa za simba ambaye ni mnyama zinajulikana kuwa ni ni mkali, mjasiri na ni mnyama ambaye anatisha sana. Kwa hivyo, Yesu ambaye ni mwana wa Mungu kulingana na imani ya kikristo ni mwenye sifa hizo kumaanisha kuwa ni shujaa wa Yuda. Maana katika usemi huu imepanuliwa kutoka kwa mnyama na kurejelea binadamu.

Katika mahubiri ambayo tulirekodi, kulikuwa na hali ya kupanuka kwa maana katika semi nyingi tulizotambua. Angalau katika mahubiri ya kila mhubiri semi zilizopanuka kimaana zilitokea. Mhubiri James Ng'ang'a katika kituo cha runinga cha KBC alitumia usemi ufuatayo katika mahubiri yake,

[11]

Wale mumezungukwa na maadui, wale mumezungukwa na watu wanaowatafuna kama big-G, wacha waendelee kuongea maana ni hawa hawa, hawa hawa ndio Mungu atawatumia kusema alikuwa haoni sasa anaona. Alikuwa haongei sasa anaongea. Alikuwa amekonda sasa amenona. Alikuwa hakuolewa sasa ameo. Alikuwa hajaolewa, ameolewa sasa.. Laana yao itawarejelea Wawa hawa ambao walikuwa wanakuambia hauwezi, upanga wa Goliathi ndio utakaomkata kichwa chake wao.

Upanga ni aina ya jisu kubwa ambalo ni pana linalotumika kukata kwa mfano miwa au mti. Pia unaweza kutumika kama silaha dhidi ya ushambulizi wa adui kwa hivyo upanga ni kifaa. Goliathi ni jina la mtu kwa hivyo ni binadamu. Kukata ni hali ya kukitumia kifaa chenye makali ambacho

ni upanga kutenganisha kitu. Hivyo kumaanisha kuwa upanga wa Goliath ni kifaa kilichotumika kumkata yeye mwenyewe.

Goliathi alikuwa mtu katika Biblia mwenye uwezo mkubwa na umbo kubwa. Alikuwa anakwenda vitani kupigana na jeshi la Israeli. Kutokana na jeshi la Israeli, mhusika kwa jina Daudi alijitolea kupigana na Goliathi kwa niaba ya waisraeli. Goliathi alikuwa na silaha nyingi zikiwemo hata upanga ilhali Daudi alikuwa tu na kombeo na jiwe moja. Katika vita, mtu mdogo Daudi alimshinda Goliathi kwa kumpiga na hilo jiwe moja na kombeo ilhali yeye alikuwa na silaha na kisha akachukua upanga wake, akamua kwakumkata kichwa chake kwa upanga huo wake.

Katika muktadha huu, upangaumelinganishwa na maovu ambayo mtu anaweza kumtendea mtu mwingineambayeni adui wake. Baadaye maovu hayo humkiukia na kumdhuru yeye mwenyewe. Jinsi upanga unavyotumika kama kifaa cha kukata unalinganishwa na maovu ya binadamu yanayomdhuru yeye mwenyewe baadaye. Maana ya upanga kama kifaa cha kukata imepanuka kimaana na kutumika kuonyesha maovu. Maana ya maneno haya inaweza kueleweka ikiwa mazingira ya matumizi yake yanaeleweka pia.

[12]

Neno upanga lilitumika na mhubiri huyu tena katika mahubiri yaleyale. Katika mfano huu upanga umetumika kwa njia tofautina ule usemiwa mhubiri katika ule mfano wa kwanza alivyotumia neno upanga.

Wakati unazuilia upanga wako usimwage damu hata kama ni ndugu yako, hata kama ni mtoto wako kumwambia ya kwamba wewe ni mzinzi na neno linakataa, wewe ni msherati hauwezi kuhudumu na mimi katika madhabahu unazuilia upanga umwage damu na unakataliwa na Mungu. Neno la Mungu ni upanga.

Neno la Mungu ni maandishi ambayo ni ya dini ya kikristo kutoka kwenye Biblia. Katika muktadha huu inaaminika kuwa Mungu huzungumza na watu kupitia kwa neno la kutoka kwenye hiyo Biblia wanayoichukulia kuwa ni takatifu. Wao huamini kuwa neno la Mungu ni Mungu mwenyewe na neno lake lina uhai. Upanga kama kifaa cha kukata kinalinganishwa na neno la Mungu. Upanga ukiwa na makali hukata chochote bila kuchagua mradi unatumika. Neno

la Mungu linalinganishwa na upanga kwa sababu linamhusumtu yeote anayelisikiliza ili kumrekebisha dhidi ya maovu bila kuchagua au kubagua ni nani anayemsikiliza na kuchagua ni nani wa kurekebisha. Kutokana na haya, neno la mungu ambalo ni maandishi kutoka kwenye Biblia inapanuliwa kimaana na kulinganishwa na upanga amba ni kifaa cha kukata.

[13]

Maandiko yananiambia siku moja akienda Damascus, Mwangaza amba ulitoka juu na ukaweza kumpiga ukamtoa juu ya farasi akaanguka chini dafrau. Huyu mtu akiwa ameanguka chini akasikia sauti ikimuuliza, ‘Sauli, Sauli, mbona wanitesa? Akauliza, ‘Ni nani ewe bwana? Nayo sauti ikamjibu, ’Ni mimi Yesu kristo ambaye unanitesa, huwezi ukaipiga miiba mateke.’

Katika mahubiri ya Pius Muiru katika kituo cha televisheni cha KBC anasema anatumia usemiulionukuliwa kutoka kwenye Biblia kuwa, huwezi ukaipiga miiba mateke. Miiba ni sehemu ya mmea yenyencha kali na ikimdunga mtu au mnyama husababisha uchungu mwingi sana na hata kuna miiba mingine ambayo huwa na sumu ambayo inaweza hata wa kuua.

Mhubiri alikuwa anamrejelea mtu katika Biblia ambaye aliiwa Sauli na aliwatesa watu wa Mungu. Mtu huyu alipokuwa akielekea mahali panapoitwa Damascus kuwatesa watu wa Mungu tena ndipo alipopigwa na mwangaza na kuanguka chini. Mungu alimwambia, Ni mimi Yesu Kristo ambaye unanitesa, huwezi ukaipiga miiba mateke.’

Wapentekoste wanaamini kuwa Mungu ana nguvu na uwezo mkubwa kumshinda mwanadamu. Kupigana na Mungu ni kama kupigana na uwezo mkubwa amba uko juu yako, kwa hivyo ni kama kukanyaga miiba ambayo inaweza kukudunga na kukudhuru. Katika ile hali ya Sauli kuwatesa watu wa Mungu, ilikuwa kama kupiga miiba mateke. Hali hii ndiyo kushindana na Mungu mkubwa ambaye ni mwenye nguvu na huwezi kumshinda. Ndio maana katika maneno hayo yanasema, mwangaza amba ulitoka juu na ukaweza kumpiga ukamtoa juu ya farasi akaanguka chini dafrau. Hivyo katika muktadha huu inaaminika kuwa ni nguvu za Mungu ndizo zilizosababisha tendo hilo. Maana katika ya usemi huu umepanuliwa ambapo, kupiga miiba mateke kunalinganishwa na kumpinga Mungu mkubwa na mwenye nguvu na uwezo mkubwa kuliko wa Mwanadamu. Usemi huuumetumika kuleta maana maalum kimkutadha.

[14]

Na tukaona alama ya nne, mwanafunzi wa Yesu Kristo anatoa mali zake kwa ajili ya kazi ya injili, bila kulazimishwa. Bila kufanya biashara na Mungu.

Mhubiri Eli Rop katika kituo cha runinga cha SAYARE alitumia usemi huu katika mahubiri yake. Alikuwa anawambia wasikilizaji kuwa, kama wanafunzi wa Yesu Kristo akimaanisha wafuasi wale ambao wameokoka watoe mali zao kwa sababu ya injili bila kulazimishwa, bila kufanya biashara na Mungu.

Neno biashara katika maana ya kawaida ni shughuli ya kununua na kuuza bidhaa kwa kupata faida. Katika muktadha huu mhubiri alimaanisha huenda mtu anatoa ili kutarajia mapendeleo au faida kutoka kwa Mungu. Wao huamini kuwa Mungu anamiliki kila kitu duniani kwa hivyo wanadamu hawezi kubadilishana chochote na Mungu. Pia wanaamini kuwa Mungu humpa mwanadamu anachohitaji kwa mapenzi yake. Wakristo wa kipentekoste wanaamini kuwa wafuasi wa Mungu wanapasa kutoa kila kitu kwa ajili ya kazi ya Mungu bila matarajio ya kurudishiwa na Mungu. Wanaamini kuwa Mungu ndiye huwapa kila kitu na anajua kile wanachohitaji. Vilevile wanaamini mali ni vitu vya dunia na vitabaki duniani. Usemi huu umepanuliwa kimaana kwa sababu mhubiri huyu hazungumzi kuhusu biashara halisi ya kununua na kuuza bali anarejelea kuhusu kutoa katika shughuli za Mungu. Mhubiri anamaanisha katika kumhudumia Mungu katika kazi yake mtu asiwe anatarajia mapendeleo au malipo kutoka kwake.

[15]

Walipokuona duni watakuwa duni wao. Maana Bwana akianza kukuinua, hakuna binadamu wala pepo anayeweza kumshawishi awache kukuinua. Atakuinua kwa sababu ye ye ni Mungu. Atakuinua kwa sababu ni mpango wake.

Neno kuinua limetumiwa mara nyingi na mhubiri huyu James Ng'ang'a katika kituo cha KBC. Kuinua ni hali ya kubeba juu kutoka katika nafasi ya chini na kusongesha katika nafasi ya juu. Katika muktadha huu anamaanisha kubadilisha hali duni na kuwa bora. Katika hali hii

wanaamini kuwa Mungu ana uwezo mkubwa wa kubadilisha mwanadamu kutoka katika hali yoyote hata iwe mbaya na hata duni na kuwa nzuri na bora zaidi. Ndiyo maana mhubiri huyu anasema kuwa ‘...maana bwana akianza kukuinua, hakuna binadamu wala pepo anayeweza kumshawishi awache kukuinua.’

Kuna kuinua kwa hali ya kubeba kutoka mahali pamoja hadi pengine kunahusishwa na hali ya kubadilika kwa maisha ambako kunachukuliwa kama hali ya kubebwa kutoka katika hali duni hadi kwa hali bora. Usemi hii unapanuliwa kimaana kwa sababu matumizi halisi ya neno kuinua yananabadilishwa kimatumizi. Katika mahubiri tuliyorekodi wahubiri tofauti amba walitumia usemi huu lakini maana yake ilibakia kuwa ileile. Mhubiri Eli Rop na Pius Muiru na William walitumia neno hilo kama ifuatavyo:

[16]

Najua katika matendo ya mitume nne kumi na mbili, si majina ya madini zetu, si majina ya maaskofu, si majina ya manabii fulani walio hapa duniani, si majina ya watakatifu fulani waliotutangulia. Hapana. Ukweli ni kwamba, Yesu ndiye njia na kweli, na uzima wa milele. Mtu haji kwa baba ila kwa Yesu. Yesu mwenyewe alisema mambo hayo. Yohana kumi nanne msitari wa sita, ‘mimi ndimi njia, ukweli na uzima’. Na inapotafuta kujua ukweli wa maneno ya Yesu Kristo, si kujiunga na dhehebu fulani. Unapotafuta kujua njia ya Yesu Kristo, si njia ya maombi fulani. Si njia ya fungu la kumi. Si njia ya sadaka. Si njia ya kufunga. Si njia ya mambo hayo yote ambayo watu wamezoa na kuleta. Ni njia ya kumwamini Yesu.

Njia ni barabara inayomuongoza mtu kutoka mahali fulani kuelekea mahali pengine. Pia inaweza kuwa namna ya kufanya jambo fulani. Lakini katika mahubiri haya, mhubiri Eli Rop katika kituo cha SAYARE anasema yesu ndiye njia ukweli na uzima. Katika muktadha huu wanaamini kuwa kuna mbingu anakokaa Mungu na kuwa wale watendao maovu hawataingia mbinguni. Katika kwenda mbinguni wanaamini kuwa mtu anaamini katika jina la Yesu na kukiri kuwa amewacha maovu. Kwa hivyo, kupitia kukiri na kuamini basi unaweza kwenda mbinguni. Kati hali hii maana ya njia inapanuliwa kulingana na maana ya kawaida ambayo ni ya kupitia na kuwa katika imani katika Yesu. Katika kumamini Yesu unakuwa na matumaini ya kwenda mbinguni. Lakini

si kwa njia ya maombi, fungu la kumi, sadaka na kufunga anavyotaja mhubiri. Hao wanaamini kuwa kupitia kwa yesu basi watafika mbinguni na kuishi maisha yasiyo na kikomo.

[17]

Mwambie mimi ni rafiki ya Mungu. Na jinsi ambavyo utaona magumu yakikukujia, hivyo ndivyo upendo wa Mungu ulio mkubwa juu yako. Na inavyozidi kuongezeka. Shetani anataka kukuonyesha Mungu hakupendi.

Katika mahubiri ya James Ng'ang'a katika kituo cha runinga cha KBC analinganisha magumu na upendo wa Mungu kwa njia isiyo wazi. Katika muktadha huu ni kumaanisha kuwa hali ikiwa mbaya ndivyo Mungu anakuwa karibu na mapenzi yake yanakuwa mengi zaidi. Katika muktadha huu wanaamini kuwa kwa sababu Yesu alikufa msalabani ili kuleta wokovu kwao, basi wao pia watateseka katika hali ya kumuamini. Kutokana na hali hii basi wanaamini kuwa mateso ni maisha ya imani yao, kumaanisha kuwa mateso yanawapa nguvu na matumaini. Kwa hivyo maana ya usemi huu imepanuka kwa sababu inachukuliwa kuwa na maana ya ndani kuliko ilivyo kwa sababu hali ngumu haiwezi kuwa inahusiana na mapenzi kwa sababu ni mambo mawili tofauti. Mhubiri huyu alitumia usemi mwagine kama huu kwa kusema kwa kusema;

[18]

Wewe ni mtu mkubwa. Magazeti itakupiga, redio zitaongea, mtaa mzima itaongea na watakuacha umesimama. Jinsi wanavyoongea kinyume chako ndivyo bwana anazidi kukuinua.

Usemi huu si wazi una maana fiche. Mhubiri huyu anaposema, "jinsi wanavyoongea kinyume chako ndivyo bwana anavyozidi kukuinua" maneno haya yanaleta maana kuwa wakati ambapo mambo au hali si nzuri, mhubiri anasema katika hali hiyo basi bwana anazidi kukuinua. Kumaanisha kuwa Mungu anaendelea kuboresha hali yako. Katika muktadha huu ni kumaanisha hali ya ugumu na kinyume ikitokea katika maisha ni kumaanisha uko karibu na Mungu. Maneno haya yametumika kuwahimiza watu wakiwa katika hali hiyo wasikate tamaa na kufadhaika lakini wawe katika hali ya matumaini kuwa mazuri yatakuja kutokea. Maana inayojitokezakatika

usemi huu ni ya kupanuka kwa sababu maana inayotokana na maneno hayo ni tofauti kimkutadha.

[19]

Mama amezaa daktari anamuuliza unasikia uchungu sana anasema sijasikia kitu. Anamuuliza kwani wewe unakuwanga na kichwa mbaya? Hausikii kitu? Akazaa mtoto wa pili hakusikia kitu. Mtoto wa tatu hakusikia kitu. Mama alisimama na microphone kutoa ushuhuda nimezaa watoto watatu bila problem na bila complication, mimi sikusikia uchungu hata ule wa kidole hivi na kisu. Naye hii ombi aliomba watu wakafikiria ni wazimu. Alikuwa anasema Jehova Mungu, wewe ulilaani wanawake na uchungu, si Yesu alisema atakuja akatoa laana.

Maneno haya ya yalijitokeza katika mahubiri ya Hurrison Ng'ang'a katika kituo cha televisheni cha MBCI. Wazimu ni mtu ambaye hana akili timamu. Mtu huyu anafanya mambo bila ufahamu na hali ya kutojua. Ombi ni njia ambayo mwanadamu huwasiliana na Mungu. Katika hali ya kawaida mwanamke akizaa husikia uchungu, lakini wapentekoste huamini katika miujiza. Miujiza ni mambo ambayo hayawezi kutendeka katika hali ya kawaida bali inatendeka mtu anapoomba kwa njia isiyo ya kawaida. Wapentekoste huwa hawana utaratibu wa kuomba. Mwanamke huyu aliomba maombi ya kukomesha uchungu wa kuzaa ambalo si jambo la kawaida. Vile ambavyo mwanamke huyu aliomba analinganishwa na wazimu. Haya yanamaanisha kuwa maombi yake hayakuwa na mpangilio na pia hakuji lewa alipokuwa akiomba. Vilevile aliomba jambo ambalo si la kawaida katika hali halisi. Maana ya wazimu imepanuliwa na kuhusisha jinsi mwanamke huyu alivyokuwa akiomba si kuwa alikuwa wazimu lakini alivyoomba alifananishwa na wazimu. Maana ya wazimu imepanuliwa kimatumizi ambapo si kuwa wazimu katika hali ya kawaida lakini ni kuomba kwa njia isiyo ya kawaida.

[20]

Kama hauwezi sema Mungu akubariki, ujiulize kama umetoa utu wa kale. Niliambiwa na mtu mwingine kwamba kuna watu ambao ungetaka kujua kama wameokoka kweli angusha shilingi. Kama hatainuka... kama shilingi ikianguka ndingli asipoinuka, utajua amekufa kweli, kwa sababu, akisikia sauti ya shilingi, hata kama atakuwa amelala, atainuka tu. Hiyo ndiyo tunaita utu wa kale. Utu wa kale wa makabila mengine

wamejaakiburi. Utu wa kale wa mahali pengine, yaani usipomsifu, wewe, usipomtambua, wewe! Ni taabu. Utu wa kale.

Mhubiri Eli Rop katika mahubiri yake anasitiza kuhusu *utu wa kale*. Mtu wa kale ina maana kuwa mtu ambaye aliishi siku za zamani. Katika muktadha wa mahubiri haya anamaanisha hali ya uovu mtu anakuwa ndani kabla ya kuokoka. Katikahali hii, ukale au uzamani unalinganishwa na uovu anaoufanya mtu kabla hajabadilika na kuwa mwema. Katika hali muktadha huu wa matumizi ni kumaanisha kuokoka. Mhubiri huyu analinganisha maovu kama ukabila, kiburi na kutomsifu Mungu akimaanisha kuwa ni kama mambo ya zamani au utu wa kale. Utu wa kale unapanuliwa kimaana na kumaanisha maovu ambayo mtu anafanya kabla ya kubadilika. Si kwamba haya ni maovu ambayo mtu alifanya zamani au kale. Katika hali hii maana ya utu wa kale unapanuliwa kimatumizi na kumaanisha maovu au utendaji dhambi kabla ya kubadilika.

[21]

Prophetically speaking, kuanzia sasa na kuendelea, hakuna wakati utakosa kuona urembo na uzuri wake Mungu ndani ya maisha yako. Financially unaenda kuona urembo na uzuri wake Jehova. Spiritually, unaenda kuona uzuri na urembo wake Jehova. In every face of your life, huenda ni medical, huenda ni social, huenda ni academic, kama vile Ayubu alivyowaona wasichana wake every day of his life, hata baada ya kuolewa.

Mhubiri Pius Muiru katika kituo cha KBC, anatumia neno urembo kwa njia isiyo ya kawaida. Neno urembo ni kitu cha kupamba, umaridadi au uzuri. Hali hii huwa ya kuvutia sana machoni mwa mtazamaji. Mhubiri huyu anaanza kwa kuwarejelea wasichana wa mtu ambaye anaitwa Ayub katika Biblia ambao walikuwa warembo sana kiumbo. Urembo unaozungumziwa mwanzoni ni urembo wa kuonekana au asili. Lakini urembo wa pili unaozungumziwa umetumika una maana isiyo ya kawaida akipanua maana yake kwa kusema, ‘Financially unaenda kuona urembo na uzuri wake Jehova. Spiritually, unaenda kuona uzuri na urembo wake Jehova’. Katika muktadha huu analinganisha mhusika Ayub katika Biblia ambaye maisha yake yalikuwa katika hali ya chini na duni lakini baadaye yakawa bora hata akapata mabinti warembo. Ule urembo wa wasichana wa Ayub ndio mhubiri anauhusisha na kumaanisha kuwa hali mbaya au duni inaweza kubadilika na kuwa nzuri, bora na ya kupendeza. Hali hiyo ndiyo anayoita

urembo kama kipesa na kiroho japo ametumia ubadilishaji msimbo wa Kingereza. Maana ya neno urembo imepanuliwa kimatumizi na kutoa maana nyingine tofauti ya mambo kubadilika na kuwa mazuri na ya kuvutia.

[22]

Sauli baada ya kuokoka, jina lilibadilika akaitwa Paulo. Mambo yote ya zamani akaachana nayo. Akaanza kuihubiri injili, mtu ambaye alikuwa akipiga injili vita. Ni yeye aliandika kitabu cha Warumi. Ni yeye aliandika kitabu cha Wakorintho. Ni yeye aliandika kitabu cha Waefeso, ni yeye aliandika kitabu cha Filipi. Ni yeye aliandika kitabu cha Timotheo.

Mhubiri Pius Muiru katika kituo cha runinga cha KBC anaposema anasema kuwa, mtu alikuwa akipiga injili vita. Vita ni mapigano ya silaha baina ya nchi, mataifa na hata wanyama. Injili ni maandishi yenje mafunzo ya dini kutoka kwenye Biblia. Maandishi hayana uwezo wa kupigana na mwanadamu. Kupigana katika vita kunalinganishwa na hali ya upingamizi au kuzuia kuendelea kwa injili katika mahubiri haya. Paulo ambaye ni mhusika katika Biblia alikuwa akiwadhulumu watu wa Mungu kwa kuwapiga na kuwatesa ili wasieneze injili. Kule kuwapiga ndiko kulikuwa kunawazuia kueneza kwa injili. Katika hali hii mhubiri huyu anasema alikuwa anapiga injili vita. Maana ya kupigana imepanuliwa kuwa si kupigana halisi bali ni kuzuia au kupinga kuenea kwa injili katika muktadha huu.

[23]

Kwa hivyo Yabesi ameitwa Yebesi kwa sababu, mama yake aliumia akimzaa. Akamwita uchungu wewe. Na kwa sababu kumwita hiyo jina, Yabesi akapatikana na mkosi kwenye maisha. Na kwa hivyo kila mkristo anayetaka kupigana na shetani lazima kwanza ajue maana ya jina lake.

Mhubiri huyu katika kituo cha televisheni cha MBCI pia ametumia neno ambalo ni kitenzi ‘kupigana na shetani’ ambapo anasema mkristo anayetaka kupigana na shetani lazima kwanza ajue maana ya jina lake. Mwanadamu hawezi kupigana na shetani kwa sababu inaaminiwa kuwa shetani ni roho ambaye haonekani na hapatikani katika ulimwengu halisi. Hali ya kupigana inayojitokeza katika muktadha huu ni kupingana na kutoshiriki kabisa katika maovu

ya kishetani. Kupigana kwa binadamu na shetani ambako kunafananishwa na kupigana kwa kawaida. Kupigana kumepanuliwa kimaana na kumaanisha hali ya kuacha au kujitenga na maovu.

[24]

Mungu ameniambia muachekufanya kesi kwa mwili mfanye kesi katika kiroho na baba amesema mfalme Mungu aishie milele amesema msikubali kesi yako ifanywe uamuzi na shetani.

Kesi ni mashtaka yaliyofikishwa mahakamani au wazee ili kusikilizwa. Maana ya kimkutadha ni kuwa changamoto na matatizo aliyo nayo msikilizaji Mungu anaweza kusikiliza kwa haki. Ni kumaanisha kuwa mwanadamu hawezu kuaminika.

[25]

I wish bwana akufungue kidogo. Unaenda mbali. I wish baba akuonyeshe kule ambako unaenda. Nikisikia magari zikiguruma, zikianza kuondoka.

Mwandishi alitumia ubadilishaji msimbo akisisitiza kuwa laiti bwana akufungue kidogo, unaenda mbali. Mbali ni kitambo kirefu baina ya mahali pamoja na pengine au mwendo mrefu. Mhubiri anapotumia neno hili anahuisha mwendo mrefu na hali ya maisha kupanuka na kuwa tofauti na kubadilika baadaye. Kwenye huu muktadha inaaminika kuwa baada ya kuokoka basi maisha yao yanabadilika hata mtu awe katika hali gani mradi uwe na imani na matumaini. Kwa hivyo hali ya matumaini ndiyo inawafanya kuamini maisha yao yatabadika na ndiyo maana mhubiri huyu anasema kuwa unaenda mbali hivyo maana ya neno mbali imepanuliwa kimatumizi.

[26]

Mimi nasikia nitabiriya kwamba familia yenu imefika wakati Mungu aanze kumkumbuka. Jehova awakumbuke as a family. Familia yenu imekuwa ni ya kufinyiliwa. Na ndio kumekuwa na vituko na visanga every time.

Mhubiri katika kituo cha runinga cha KBC anatumia kufinyiliwaambalo linamaanisha kumininga kwa vidole. Katika muktadha huu mhubiri huyu anahuisha na hali ya kunyanyasa, kudunishwa na kuumizwa kama ya kufinyiliwa hivyo maana yake imepanuliwa kimatumizi hivyo kumaanisha kunyanyaswa na kudunishwa.

[27]

Wakati mzee alimwuliza, ‘Sasa Esther, sema unataka nini?’ Esther alijua, nusu ya tumbo iko na chakula ya miungu mingine, na nusu ndio iko na yangu. Akamwambia mzee kama unanipenda, tena kesho, kujeni *dinner*. *Dinner* ya pili wakato walikuja ndio Esther alitoa rangi zake

Mahubiri haya yalitoka kwa mhubiri Benson Ng’ang’a. Rangi ni sura kitu kinavyofanana. Esther kutoa rangi yake ni kumaanisha sasa alikuwa mwenyewe asili au kuwa mkweli yaani kusema ukweli uliokuwa ndani ya moyo wake. Maana ya rangi inapanuliwa na kumaanisha hali yake asili au hali yake ilivyokuwa.

[28]

Mtu anapozaliwa mara ya pili, unaposamehewa dhambi zako, bibilia inasema kwamba, imekuwa basi, mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipyta, ya kale yanapita. Tazama yote yanakuwa mapya. Paulo akatilia mkazo zaidi akifundisha. Akasema basi kama umezaliwa mara ya pili, kwa kumwamini Yesu Kristo. Katika wakolosai tatu kuanzia aya ya tano, akasema, basi, ueni, angamizeni, malizeni tabia yenu ya zamani iliyo katika miili yenu. Akaanza jambi usherati, uchafu, akaendela, na akaendela, na akaendelea mpaka akamalizia ibaada ya sanamu. Kuua, kumaliza.

Ua ni kitendo cha kutoa uhai wa mtu au kiumbe kingine kwa kukusudia au kwa ajali. Neno hili lina maana ya kupanuka vilevile kubanika. Kwa sababu maana yake imepanuliwa kimatumizi na kuhusisha kuua kwa tabia. Lakini pia kuua ni kufisha au kukomesha hali fulani. pia unaweza kuua mwenendo au tabia ndani ya mtu kumaanisha kukomesha au kufisha ili isionekane tena. Katika muktadha huu mfasiri anaacha maana ya kiumbe au binadamu kupoteza uhai bali anachukua maana ya kupotea au kukomesha kabisa. Maana ya kuua ni kuondoa kuwepo kwa uhai

au kuwepo kwa hali. Katika muktadha huu maana inabanika kwa kukomesha kuwepo kwa hali. Sitiari hii ilijitokeza katika mahubiri ya Eli Rop katika kituo cha runinga cha SAYARE.

[29]

Uende ukiua bila huruma.uue hata kama ni ndugu yako, hata kama ni mtoto wako ye yote utakayepata ua

Mhubiri William katika kituo cha MBCI anatumia kitenzi ua lakini katika muktadha mwingine kwa njia wazi.

[30]

Bibilia inasema makutano ya watu wengi wanamfuata Yesu. Yesu akajua hawa wanani fuata, hawanijui. Hawa awananifuata, hawajui vile mimi huwa nataka. Yesu akawageukia makutano. Akasema, unataka kunifuata? Mtu ye yote anataka kunifuata lazima achukie baba yake, achukie mama yake, achukie watoto wake, achukie ndugu zake, achukie dada zake, hata ye ye mwenyewe ndio aweze kunifuata. Na wakati mwingi huwa tunashindwa namna hivyo. Siyo rahisi kuchukia baba na mama. Siyo rahisi kuchukia ndugu yako.

Mhubiri Wiliam.J. katika kituo cha runinga cha MBCI anatumia neno chukia mara kadha. Kuchukia ni kupoteza mapenzi kwa mtu au hali ya kuwa na roho mbaya au kuwa na kinyongo. Si rahisi katika hali ya kawa idha mtu kuwa na chuki kwa ndugu yake, dada yake na watoto wake. Vilevile mafunzo ya kiblia huwa yanapinga chuki kwa sababu huo ni uovu amba o unachukuliwa kama dhambi. Katika hali ya kawa idha binadamu hupatikana au huendeleza uovu. Kipentekoste inaaminika kuwa Yesu ni mtakatifu. Kwa hivyo katika muktadha huu inamaanisha kuwa yesu ni mtakatifu na ye yote anayemfuata ni lazima awe mtakatifu. Mtu kuwa mtakatifu ni lazima ufuatempenzi ya Mungu lakini si ya binadamu hata awe ndugu yako, dada yako na watoto wako. Hao wanaamini kuwa binadamu anaweza kuingiwa na maovu. Hapa maana ya neno kuchukia limepanuliwa kimaana ili kumaanisha kujiepusha na wale wanaotenda maovu ambayo ni kinyume na mapenzi ya Mungu.

[31]

Kwa sababu Biblia inasema iwapo unamchukia mwenzako wewe ni muuaji.

Katika usemi huu huu mwenendo wa kutompenda mtu unalinganishwa na kuwa muuaji. Mhubiri huyu anasema iwapo mtu anamchukia mwenzake analinganishwa na muuaji. Katika muktadha huu chuki inachukuliwa kama tendo la uovu ambalo linaweza kukata uhusiano kati ya watu. Kukatika kwa uhusiano kati ya watu kunazuia mambo mengi kuendelea kati ya watu hivyo basi ni kama kufa. Kwa hivyo maana ya muuaji impanuliwa na kuhusisha mtu ambaye anamchukia mwenzake katika muktadha huu.

Mhubiri Eli Rop katika kituo cha runinga cha SAYARE anasema haya,

Mimi ni ng'ombe

Utu wa kale wa mahali pengine yaani utu wa kale. Mtu mwingine akakasirika ati ameitwa Ng'ombe mpaka akafanya vita ati kwa sababu ameitwa ng'ombe. Na kusema ng'ombe mara mia moja, ng'ombe ukifikiri mimi ni ng'ombe.

Ng'ombe ni mnyama anayefugwa na binadamu. Mnyama huyu ni wa manufaa kwa binadamu, kwa sababu anampa nyama, maziwa, na hata kufanya kazi kama ya kulima shambani. Hata hivyo ng'ombe hana ufahamu kama wa mwanadamu kwa sababu ni mnyama. Lazima aelekezwe na binadamu ili aweze kutekeleza majukumu yake na pia wakati mwingine anaweza kuwa mnyama mwenye ujeuri, kukasirisha, mtundu na hatari.

Katika muktadha huu mhubiri huyu anahuishwa binadamu na ng'ombe ambaye ni mnyama. Kwasababu anasema mtu mwingine anakasirika ati anaitwa ng'ombe anarejelea sifa mbaya ya ng'ombe ambayo si nzuri bali mbaya ya kutokuwa na ufahamu na ujeuri. Katika hali hii maana ya ng'ombe kama mnyama inapanuka na kuhusishwa na binadamu.

[32]

Eli ni mungu

Maneno haya yalitokea katika mahubiri ya mhubiri Harrison Ng'ang'a katika kituo cha runinga cha MBCI. Mhubiri Hurrison Ng'ang'a ansema 'Eli ni Mungu'. Katika hali halisi Mungu ni

mmoja na Eli ni mhusika katika Biblia ambaye analinganishwa na Mungu. Mfalme Nebuchadnezar alijua siri ya jina kama hili. Kwa sababu alisema, wewe unaita Danieli? Ee Danieli ni kusema mungu wa mbinguni, Dan unaelewa ni kusema watu wale wamebarikiwa pale na baraka za hapa duniani.

Mungu anafikiriwa kuwa mkuu wanatheolojia wamemueleza kama mwenye maarifa, mwenye kuwa kila mahali na mkamilifu. Mungu ni muumba na mhimili wa vilivyoumbwa. Danieli alikuwa mtu tu mwenye maarifa na hekima kama ya Mungu. Vilevile alikuwa mtu ambaye alikuwa amefanikiwa pakubwa na hata aliheshimiwa na utawala uliokuwepo wa mfame Nebuchadnezar. Ukuu wa Danieli unahushwa na ukuu wa Mungu ndio maana mhubiri anasema kuwa Danieli au Eli ni Mungu. Usemi huu unaleta kupanuka kwa maana ambapo ukuu wa Mungu unahamishwa na kumrejelea Danieli ambaye ni binadamu.

[33]

Tukaangalia kwamba alama ya kwanza ni mtu kuzaliwa mara ya pili kwa kutubu dhambi zake kwa kugeuka

Kuzaliwa mara ya pili katika hali ya kawaida ni kutoka tumboni mwa mama yako urudi ndani tena uzaliwe mara nyingine. Katika hali halisi kitendo hiki hakiwezekani, mhubiri huyu hakumaanisha kufanyika kwa kitendo hicho cha kuzaliwa mara ya pili. Lakini alimaanisha kuwacha dhambi ambazo ni mambo maovu kabisa na kuanza kuishi maisha mapya bila lawama. Hali hii huchukuliwa kuwa ni kuokoka na kujitenga na maovu kabisa. Usemi huu umepanuliwa kimaana kwa sababu maana ya kawaida ya kuzaliwa mara ya pili kunaleta maana ya kuwacha kutenda maovu na kutenda mema.

[34]

Kusulubisha mwili

Neno hili kusulubisha lilitokana na kusulubishwa kwa yesu vile alivyopigiliwa na misumari msalabani. Baada ya kusulubishwa yesu alizikwa na kufufuka akiwa na uhai mpya. Katika

muktadha huu ni kumaanisha kufisha, kuua na kujitenga na maovu. Kule kujitenga na maovu ndiko kusulubisha mwili. Baada ya yesu kusulubishwa na kufa, ndipo uhai wa mwanadamu ulipatikana kulingana na imani ya kipentekoste. Kuna hali ya ulinganishi kati ya kufa kwa yesu msalabani na kufa kwa hisia za kimwili zimwingizayo mtu katika maovu hivyo ni kama kuzisulubisha. Katika usemi huu kuna kupanuka kwa maana kwa sababu maana ya neno kusulubishwa imepanuka na kuitumia kwa maana nyingine ya kuua hisia za kumwezesha mtu kuingia katika maovu. Baada ya kuufisha mwili na kujitenga na dhambi ndipo mtu anaanza mwanzo mpya.

[35]

Alimwambia mtakuwa mkitembea hivi mkiomba mkate.

Mkate ni chakula kinachoundwa kwa unga wa ngano, chachu na maji. Katika muktadha huu haimanishi kuomba mkate huu bali ni mahitaji yote ya kila siku au chakula cha kila siku. Maana ambayo imejitokeza hapa imepanuliwa ambapo maana ya mkate imepanuliwa katika matumizi kuleta maana chakula au matumizi ya kila siku.

[36]

Kuwachota

Kuchota ni kuchukua sehemu ndogo ya kitu kwa mfano maji, unga kwa kiganja au chombo. Maana inayojitokeza ni kuwa hali ya kuchukuliwa kwa wingi. Maana ya neno hili inapanuliwa kimatumizi kumaanisha washirika wanachukuliwa na wahubiri wa makanisa mengine. Katika hali halisi wanadamu hawawezi kuchotwa.

[37]

Ninajua umesikia maneno mengi na kwa sababu ulitilia maanani ikazaliwa kwa anga yako.

Katika mahubiri ya Ng'ang'a anatumia anatumia usemi huu. Anga ni uwanda ulio juu mbinguni. Anga inalinganishwa na hali kuyashika maneno na kuyakubali yakakaa akilini mwa mtu kwa hivyo akilini mwa mwanadamu mnahusishwa na anga. Hali inayojitokeza katika usemi huu ni kupanuka kwa maana.

Tashihisi

Ni hali ambapo vitu ambavyo havina sifa ya kibinadamu vinapewa sifa ya kibinadamu. Mhubiri James Ng'ang'a katika kituo cha KBC anatumia huu mfano;

[38]

Na jinsi ambavyo utaona magumu yakikukujia, hivyo ndivyo upendo wa Mungu ulio mkubwa juu yako. Na inavyozidi kuongezeka. Shetani anataka kukuonyesha Mungu hakupendi. Wewe ni mtu mkubwa. Wi mundu munene. Wewe ni mtu mkubwa. Magazeti itakupiga, redio zitaongea, mtaa mzima itaongea na watakuacha umesimama. Jinsi wanavyoongea kinyume chako ndivyo bwana anazidi kukuinua. Watapigana na wewe, na hawatakuweza.

[38b]

Magazeti yatakupiga

Kifungu hiki kimetolewa katika mahubiri ya James Ng'ang'a katika kituo cha runinga cha KBC. Katika tashihisi hii, magazeti ni karatasi ambazo hazina uwezo na ufahamu wa kupiga, ilihali yamepewa uhai na uwezo wa kupiga. Katika hali ya kupiga kunaweza kuwa na uchunguunaotokana na kipigo. Magazeti yatakupiga ni kuonyesha kuwa magazeti yanasantaza ujumbe ambao huenda utakuumiza kiakili na ndiyo hiyo hali inayohusishwa na kipigo halisi. Hali ya kupiga inayohusishwa na kiumbe chenye uhai inatumika kwa kitu kisicho na uhai na kupiga.

[39]

Redio zitaongea, mtaa mzima itaongea na itakuwacha umesimama

Redio ni chombo kilichotengenezwa na binadamu na hakina uwezo wa kuzungumza. Mtaa ni mahali ambapo ni ombwe tupu. Kuongea kwa binadamu kunalinganishwa na redio kusambaza ujumbe na watu wanavyosambaza ujumbe mtaani baada ya kuupata. Neno kuongea limepanuliwa kimaana ambapo mitaa imepewa uwezo wa kuongea kama binadamu.

[40]

Maandiko yananiambia aliposimama macho yake yakawa hayaoni

Maandiko ni mandishi ambayo hayana uwezo wa kusema na mtu. Katika mahubiri ya Pius Muiru yanaonyesha kuwa maandishi yana uwezo wa kusema lakini ni kuonyesha ufahamu anaopata kutoka kwenye ujumbe ulio kwenye maandishi. Maana ya tashihisi hii imepanuliwa kimatumizi ambapo maandishi yanapewa uwezo wa kuongea.

[41]

Hata kama ni ndugu yako hata kama ni mtoto wako kumwambia ya kwamba wewe ni mzinzi na neno linakataa wewe ni msherati hauwezi kuhudumu.

Neno ambalo ni maandishi pia linapewa uwezo wa kupinga au kukataa. Maana yake inapanuliwa kimatumizi. Mmhubiri anamaanisha kuwa tabia ya uzinzi anayozungumzia ni kinyume na neno la Mungu ambalo linachukuliwa kuwa takatifu

[42]

Hii biashara yako umeongelesha kila wakati.

Katika tashihisi hii biashara ambayo ni kazi imehuhishwa. Maana ya kuongea inayotokea kati ya binadamu imehusishwa na biashara hivyo kupanua maana yake kutoka kwa maana ya kawaida.

[43]

Pastor anataka kanisa inenepe kidogo anaona inarudi chini

Kunenepa ni hali ya kunawiri na kuongezeka kwa umbo. Hii ni hali ambayo inaweza kutokea tu kwa kiumbe au kitu kilicho na uhai bali si kwakanisa ambalo ni jengo. Kuna hali ya kulihusishai kanisa na kiumbe au kitu kilicho na uhai kumaanisha hali ya kuongezeka. Hali ya kunenepa

inayohusishwa na binadamu imepanuliwa kimaana ili kuhusisha kanisa ambalo ni jengo. Vilevile kihalisia jengo haliwezi kunenepa mhubiri huyu anamaanisha idadi ya watu kuongezeka katika jengo hilo.

3.2.1 Mbazi

Mbazi hutumika kuelezea hadithi au kisa ambacho kinazungumzia mtu, watu au tukio fulani ingawa maana inayolengwa huwa ya ndani. Katika mfano kwenye mahubiri ya Pius Muiru katika kituo cha televisheni cha KBC anasema;

[44]

Sasa tunaangalia katika kitabu cha Ayub chapter 42 naverse number 15 mahali nenolinatuambia kwamba alikuwa na wasichana warembo sana. Wasichana watatu wa Ayubu majina yao yamepeanwa na katika majina hayo msichana wa kwanza anaitwa Jemima. Msichana wa pili anaitwa Keziah na msichana wa tatu anaitwa Kellen Hapuch.

Jina Jemima ni day by day, msichana wa pili anaitwa Keziah ni ile spice inafanana na cinnamon inaitwa cassius. Kezia ni spice na inafanya chakula iwe ya kutamanika. Msichana wa tatu anaitwa Kellen Hapuch maana ya jina Kellen Hapuch ni kifaa ambacho kina dada wa nchi ya mashariki walikuwa wanatumia ku apply wanja kwa macho yao kwa ajili ya kujirembesha

Kutokana na mbazi hii, ujumbe wake si wa moja kwa moja. Kuna mafunzo yanayotokana na majina ambayo wahusika walipewa kwa hivyo yalikuwa majina ya kiishara. Majina waliyopewa binti za Ayubu yalikuwa na maana yake maalumu. Katika mbazi hii ya kibiblia kisa kilichompata Ayub kilikuwa na ujumbe wa ndani kwa sababu mhubiri hakumaanisha hadithi hii ilivyowasilishwa moja kwa moja bali aliipanua kimatumizi na ikawa na ujumbe tofauti ulivyowasilishwa kutoka kwenye Biblia. Kwa mfano Kezia linamaanisha viungo vinavyoongezwa kwa chakula ili kuongezwa ladha. Kellen Hapuch maana yake ni vitu vyatujirembesha. Kutokana na mbazi hii mhubiri anazungumzia urembo ambao si halisi bali hali katika maisha kubadilika na kuwa ya kupendeza.

[45]

Matendo ya mitume chapter number nine.

Kuna mtu ambaye anaitwa Sauli ambaye alikuwa na contingent yake alikuwa na kikosi ambacho alikuwa anazunguka nacho. Akipata mahali mukutano inahubiriwa ya crusade anaisambaratisha na anawakamata wahubiri na ushers.

Siku moja akienda Damascus mwangaza ambaa ulitoka juu na ukaweza kumpiga ukamtoa juu ya farasi. Huyu mtu akiwa ameanguka chini akasikia sauti ikimuuliza Sauli Sauli mbona wanitesa? Akauliza ni nani ewe bwana? Nayo sauti ikamwambia Ni mimi Yesu kristo ambaye unanitesa. Huwezi ukaipiga miiba mateke Aliuliza unataka nikufanyie nini? Akaambiwa simama nenda Damascus utaambiwa upasavyo kufanya. Aliposimama macho yake yakawa hayaoni. Kwa muda wa siku tatalipoteza uwezo wa kuona. Macho yake yalipotea akawa hawezi akaona.

Hii ni mbazi nyingine inayojitokeza katika mahubiri ya Pius Muiru. Anazungumza kuhusu mtu ambaye anaitwa Sauli. Mtu huyu alipokuwa akiwadhulumu watu wa Mungu anapigwa na mwangaza uliomtoa juu ya farasi. Kitendo hiki ni cha maana ya ndani, kuwa huwezi kupigana na nguvu zinazokushinda. Inaaminika kuwa Mungu ana nguvu kuu kumshinda mwanadamu.

[46]

Mtu ambaye hapo awali alikuwa adui ya msalaba. Alikubali Mungu ambadilishe, Jehova alimbadilisha na new testament (agano jipy) yote imeandikwa na huyo mtu.

Kuna neno msalaba lililotumiwa na huyu mhubiri katika kituo cha runinga KBC. Msalaba ni kipande kinachoundwa kutokana na mbaa ambacho kinajulikana kuwa ni ishara ya ukristo. Lakini neno hili msalaba lina uzito na maana ya ndani kwa wapentekoste. Inaaminiwa kuwa Yesu mwana wa Mungu alisulubishwa msalabani na kule kusulubishwa msalabani kulileta msamaha wa dhambi ili kuleta mwanzo mpya kwa mkristo. Pia inaaminika kuwa msalaba unaleta hali ya kubadilika ambayo ni kuokoka na kupata urejesho wa mwanadamu kutokana na maisha ya uovu. Inachukuliwa kuwa msalaba huleta ukombozi unaomfanya mtu anatengana na dhambi kabisa kwa muktadha wa kipentekoste.

Katika matumizi yake katika mahubiri, mhubiri anasema kuwa, mtu ambaye alikuwa adui wa msalaba, alikubali Mungu ambadilishe. Maneno haya yanamaanisha kuwa mtu huyu alikuwa muovu sasa amebadilika na kuwa mtu mwema kwa sababu ya msalaba. Kwa hivyo maana ya

msalaba katika mukutadha huu si tu alama ya ukristo inavyochukuliwa katika hali ya kawaida bali ina maana ya mabadiliko makubwa katika imani ya mpentekoste. Maana ya msalaba si tu ukristo bali inabeba uzito zaidi ya inavyochukuliwa na watu wengine wasio na imani hii.

[47]

Njia ya kuingia kwa moyo wa mwanaume ni kupitia kwa tumbo. Na ndio watu wengi wanapenda kununulia wanawake wa wenyewe chai, uji na kahawa. Mama ya wenyewe akikunywa kahawa yako na uji na nini, sasa ameanza kukufuata. Kwa hivyo ukiona mtu anataka kukununulia chai mwambie am sorry, nitakunywa nyumbani, Mungu akubariki. Kwa hivyo Yabesi alikuwa na *a curse on him*. Bibilia inasema... Bwana asifiwe... unajua wakati wa Yabesi si kama sasa, sasa tuko na damu ya Yesu, tunaweza ku-reverse mambo mengi.

Usemi huu ulitumika katika mahubiri ya Hurrism Ng'ang'a katika kituo cha MBCI. Mhubiri huyu alitumia usemi wa damu ya Yesu ambayo ni maji mekundu yanayozunguka kwenye mishipa ya kiumbe na ni ya muhimu sana kwa uhai mwilini mwa binadamu. Uko sefu wa damu mwilini huonyesha dalili ya hatari kwa uhai wa mwanadamu.

Katika muktadha huu damu ya Yesu ni ile damu ambayo Yesu ambaye ni mwana wa Mungu alimwaga msalabani aliposulubishwa. Yesu alisulubishwa msalabani kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu. Damu hii katika hali hii ina uzito na maana ya ndani. Kwao wanaamini kuwa damu ya Yesu ina maana ya kusafisha na kutakasa ili kufanya safi maisha ya mwanadamu. Hii inamaanisha kuwa ina uwezo wa kuosha na kuondoa maovu kwa wale wenye hiyo imani. Damu ya Yesu ni inasimamia msamaha na utakaso kwa sababu wanaamini kuwa bila damu ya yesu kristo hakuna msamaha na wokovu kwao. Pia inaaminika kuwa damu ya Yesu inawapa uhai wa kiroho na ushindi wa kukabiliana na hali ngumu katika maisha na ndio maana mhubiri anasema kuwa sasa tuko na damu ya Yesu, tunaweza ku-reverse (maana ya kubadilisha) mambo Ametumia ubadilishaji msimbo katika Kingereza kumaanisha damu ya Yesu ina nguvu ya kubadilisha mambo hata yawe mabaya kiasi gani. Kwa sababu hiyo damu ina nguvu za kiungu zinazoweza kubadilisha hali. Maana yake imepanuliwa kimaana.

[48]

Jiachilie sasa, toka kwenye haya maroho uliambiwa na uanze kujiambia, uanze kusema I am a winner, I am going to win this battle. I am going to conquer. Ninaenda kupeperusha bendera katika familia, kama vile Daudi alifanya. I am going to sing many songs.

Mhubiri huyu ametumia usemi wa bendera ambayo ni ishara. Bendera ni kipande cha nguo kinachotumika kama ishara inayotoa ujumbe fulani na wakati mwingine hutumika kama maridadi. Bendera ya kitaifa hutumika kama alama ya fahari, uzalendo na heshima kwa nchi. Pia bendera inaweza kutumika kuonyesha amani, umoja na ushindi.

Katika muktadha huu mhubiri huyu anazungumza kuhusu hali ngumu kutokea ambazo anaziita vita za kupigana, hata hivyo anawahakikishia wasikilizaji watakumbana na hali hizo wameshinda tayari. Neno bendera katika hali hii huu limetumika kuashiria ujasiri na ufanisi kutokana na hali na vita vigumu anavyozungumzia mhubiri huyu. Anasema kuwa watapigana na wewe na hawatakuweza. Baada ya kupigana na kupata ushindi mtu anakuwa na fahari, ushindi huo utaweza kusimama na kuonekana na kila mtu kama vile bendera inavyoonekana. Kimuktadha Daudi alipigana vita vigumu na akashinda kisha akapeperusha bendera ya ushindi. Bendera ni usemiwenye uzito ndani yake. Kabla ya kupeperusha bendera huwa kumekuwa na kuna hali ngumu inayotokea kwanza. Maana ya bendera imepanuliwa kimatumizi kwa sababu maana yake ni tofauti na maana yake asili.

[49]

Maandiko yananiambia siku moja akienda Damascus, mwangaza ambao ultoka juu na ukaweza kumpiga ukamtoa juu ya farasi. Akaanguka chini dafrau. Huyu mtu ikiwa ameanguka chini, akasikia sauti ikimuuliza, ‘Sauli Sauli, mbona wanitesa?’ Akauliza, ‘Ni nani ewe bwana?’ Nayo sauti ikamwambia, ‘Ni mimi Yesu Kristo ambaye unanitesa.

Mwangaza ni nuru ya juu au taa. Mahali ambapo kuna mwangaza hakuna giza, pia mahali pale pana uhai na matumaini. Katika muktadha huu, mwangaza umetumiwa kwa njia isiyo ya kawaida ya kumpiga mtu na kumbeba. Mwangaza ni unawakilisha nguvu za Mungu na Roho Mtakatifu. Katika muktadha huu mwangaza ni ya uwepo wa Mungu. Katika hali ya kawaida mwangaza hauna nguvu za kuweza kumbeba mtu kutoka mahali pamoja hadi pengine. Lakini

tunaambiwa kuwa mwangaza ambao ultoka juu na Sauli kumpiga ukamtoa juu ya farasi. Maana ya neno hili imepanuliwa kwa sababu maana ilivyotumika si kama inavyoilewaka katika hali ya kawaida. Katika hali hii si kwamba mwangaza ambao ni nuru ndiyo uliompiga Sauli na ukamtoa kwenye farasi bali zilikuwa ni nguvu na uwepo wa Mungu. Mwangaza unawakilisha nguvu, uwezo na uwepo wa Mungu.

3.3 Kukisia kwa maana kwa semi katika mahubiri

Huu ni ya ukadiriaji wa hali. Ufasiri ambapo neno lenye maana finyu linapanuliwa kimaana ili kuhusisha maana ya kitu kinachohusiana nacho ambacho kina maana tofauti na maana halisi ya neno hilo kiisimu. Kwa mfano, Musa ambaye alikuwa anahitaji shilingi mia tano ili atumie kutekeleza shughuli fulani. Akisema nikipata shilingi mia nne zitanifaa, atakuwa anakisia tu kwa sababu alikuwa anahitaji shilingi mia tano wala si mia nne.

[50]

Kusema kwamba sasa tukitenga watu, watu wengine wako tayari kuwapokea. Ukijaribu kusema kwamba huu ndio utakatifu, watu wengine wako tayari kuwachota. So unakuta kwamba, hata wale ambao wangehubiri ukweli, wameanza kuogopa kuhubiri ukweli. Na hapo ndipo tumeanza kukubali mambo yasiyo safi katika nyumba ya Mungu. Lakini tunasahau ya kwamba, tunaweza kuwapata watu katika makanisa yetu. Tunaweza kuwajaza watu elfu elfu. Tunaweza kuwajaza watu mpaka unakuta kwa kanisa watu elfu mia tatu, watu milioni moja. Tunaweza kuwajaza

Maneno haya yalijitokeza katika mahubiri ya Eli Rop kwenye kituo cha runinga cha SAYARE. Maneno haya yanaleta kukisia kwa maana pasipo kutaja idadi dhahiri. Mhubiri huyu aliyasema maneno haya akimaanisha kuwa wahubiri wengi wanahubiri mahubiri ya kuwafurahisha watu ili waje wengi wajae kanisani. Lakini mhubiri huyu alikuwa anasema wanaweza kuhubiri mahubiri safi na bado yanaweza kuwavutia na kuwaleta watu wengi kanisani. Maneno haya yanaleta uhusiano wa kiadidi ambao mhubiri anazungumzia kuhusu wingi wa watu wanavyoweza kujaa kanisani kunaweza kuwa na watu wengi kanisani. Katika kuzungumzia wingi wa watu ndio anasema kwa kukisia tu; Tunaweza kuwajaza watu elfu elfu kuwajaza mpaka kwa kanisa watu elfu mia tatu, watu milioni moja.

[51]

hawa wasichana kama ni wakati wa kuolewa, ilibidi wenye kuwaoa wakuje kwenye inheritance ambayo waligawiwa na baba yao. Yaani, Ayubu alikuwa ni billionaire. Wasichana wake akawagawia estates zake. Wenye kuwaoa itawabidi waje mpaka huku. Maana yake ni nini? Ni ya kwamba Ayubu alikuwa anawaona wasichana wake warembo every day of his life.

Mhubiri Muiru alitumia maneno haya kwa kukisia tu. Anamrejelea mhusika katika Biblia anaaitwa Ayub ambaye alipitia hali na maisha magumu. Alipoteza mali yake yote lakini baadaye mambo yakambadilikia na mali yake ikarejea na kuwa nyingi sana. Mhubiri aliposema kuwa Ayub alikuwa billionaire anahusisha na wingi wa mali aliyopata Ayub baada ya kupitia hali ngumu katika maisha kwa kukisia tu.

[52]

Mfululizo wa mafundisho niliyoyatilia mkazo sana ambayo kwa upande mwingi kanisa ni kama tulianza kusahau. Kwa sababu tulianza kuona kanisa kama ilivyo tukaangalia upande mmoja. Si upande mbaya, upande wa kubarikiwa, upande wa kuomba miujiza na ishara. Ni vizuri. Ukaanza kuona ni kama tulianza kuelekea zaidi upande huo, kuliko kuangalia shabaha kamili ya ndani. Tukasahau ya kwamba, hata miujiza ilioje inaweza kutendeka na zinaweza kukuacha. Hata Mungu akikupatia bilioni mia moja leo, ni pesa ambazo zitabaki dunia. Hata ukijenga magorofa, itaisha kwa sababu parapanda itakapolia, utanyakuliwa.

Mhubiri huyu anaposema pesa bilioni moja ni kumaanisha kuwa hata akipewa kiasi kikubwa cha pesa hakuna kutosheka na hazina maana yoyote. Kwa hivyo bilioni moja inahusishwa na kiasi kikubwa cha pesa anachoweza kupata. Maana inayojitekeza katika usemi huu ni ya kukisia tu.

[53]

Ukiona ndugu kila mnaenda mahali anakula nyama kilo moja na mfuko mmoja ya ugali ile ya kilo mbili, anakuambia wakati wa kukula ni wakati wa kukula.

Mhubiri William katika kituo cha MBCI anapotumia maneno haya ambapo Biblia inasema kuwa ikiwa mtu ni ndugu hapaswi kuwa mlafi. Ametumia maneno haya yametumika kuonyesha kiasi cha chakula ambacho mtu ambaye ni mlafi anaweza kula kwa kukisia tu

[54]

Mimi naona mahali tunapitia kama taifa ni wakati ambapo watu wengi hata watumishi wa Mungu watapoteza kibali cha bwana. Hata washirika wa makanisa watu ambao wameitwa watapoteza kibali cha bwana, *because* ninaona ya kwamba ni wakati ambapo Mungu anajaribu mioyo ya watu.

Mhubiri huyu anazungumza kuhusu watu wa Mungu kupoteza kibali katika enzi tunazoishi. Katika kuzungumza kuhusu idadi ya watu kupoteza kibali, anakisia tu kwa kusema kuwa watu wengi hata watumishi wa Mungu watapoteza kibali cha bwana, bila kusema idadi kamili.

3.4 Kubanika kwa maana katika semi

Hali hii hutokea ambapo neno lenye maana pana linatumika kuonyesha maana finyu ya neno hilo. Kwa mujibu wa Wamitila, (2008:79) hali hii hutokea pale ambapo maana ya neno hufinywa na kuacha kutumika kwa maana nyingi. Ufinskyaji wa kimaana hutokea pale ambapo maana moja maalum ya neno inatawala na kuishia kuifanya au kuzifanya maana nyinginezo na neno maalum kufifia na labda hata kupotea kabisa. Mifano mingi semi zilizotumika katika mahubiri tuliyorekodi zimepanuliwa kimaana. Hata hivyo ni semi chache sana ambazo zilibanika kimaana.

[55]

Na jinsi ambavyo utaona magumu yakikukujia, hivyo ndivyo upendo wa Mungu ulio mkubwa juu yako. Na inavyozidi kuongezeka. Shetani anataka kukuonyesha Mungu hakupendi. Wewe ni mtu mkubwa. Wi mundu munene. Wewe ni mtu mkubwa. Magazeti itakupiga, redio zitaongea, mtaa mzima itaongea na watakuacha umesimama. Sitiari hii inamaanisha kuwa kutakuwa na mabadiliko kutoka kwenye hali ya udogo na kuwa katika hali ya ukubwa.

Kubwa ni kuu kimaumbile au urefu au upana usio kidogo, enye miaka mingi, iliyopata kukua au yenyе hali ya juu. Mhubiri huyu James Ng'ang'a katika kituo cha runinga cha KBC katika muktadha huu alitumia usemi huu kumaanisha kuwa hali kubadilika kutoka kwenye hali duni. Kwa hivyo maana zingine za umbo au urefu, upana, miaka mingi kisha kuchukuwa maana ya hali ya juu.

[56]

Pastor anataka kanisa inenepe kidogo anaona inarudi chini.

Kunenepa ni hali ya kuongezeka kwa umbo pana au kujaa. Viumbe au vitu vingi vinaweza kuwa vikubwa lakini katika muktadha huu maana ya kuwa kubwa imebanika kwenye kanisa.

[57]

Leo hii, ningependa kujenga zaidi tena, kwa sababu tutaendelea na masomo hayo ya shabaha ya injili ya Yesu Kristo kwa kipindi kile roho mtakatifu atakavyotuwezesha.

Nasikia sauti... wengine wakisema, kama ni namna hiyo, heri, itakuwa ngumu kuingia mbinguni. Sio hivyo! Si Bibilia inasema kwamba njia ile ya kuenda mbinguni, barabara ni nyembamba sana na wachache wanaipata. Kumaanisha kuna wale watakaoipIta. Ni ukweli kwa wale wanaosikia mafundisho haya ambayo ninafundisha leo ambayo yananenwa na roho mtakatifu.

Neno hili liliyotumiwa na mhubiri Eli Rop. Roho mtakatifu ni roho Katika muktadha huu ni roho mwenye nguvu za kiungu na huchukuliwa kama mtu wa tatu katika hali ya utatu katika imani ya kikristo. Roho mtakatifu huchukuliwa kuwa ni mtu na ni mwenye ukweli kwa sababu anawambia ukweli katika imani yao kutoka kwa Mungu na inaaminiwa kuwa anaishi ndani ya mwanadamu. Si kila mtu anapokea roho mtakatifu bali wale ambao ni safi kumaanisha wameokoka na inajidhihirisha kupitia kuongea katika lugha ya kiungu isiyoleweka inayoitwa ndimi.

Roho mtakatifu ni neno linaloleta kubanika kwa maana kwa sababu dini zingine zinatumia ishara hii katika mahubiri au katika imani yao kama dini ya kiislamu, Bahai na dini ya Uyahudi. Katika muktadha huu Roho mtakatifu inaaminiwa kuwa ni Mungu anayeishi ndani ya wakristo walio okoka na huathiri mawazo na kufikiria kwao. Pia wanaamini kuwa roho mtakatifu huwapa mwelekeo kuhusu kile wanachopasa kufanya. Katika mifano yetu mhubiri huyu anasema ataendelea na mahubiri wakati mwingine vile roho mtakatifu atakavyomuezesha. Anaendelea kusema kuwa ni ukweli kwa wale wanaosikia mafundisho haya ambayo ninafundisha leo ambayo yananenwa na roho mtakatifu. Matumizi ya roho mtakatifu kama imebanika kimaana kulingana na kanisa la kipentekoste kwa sababu dini zingine pia zina roho mtakatifu na anavyochukuliwa na kumaanisha ni tofauti katika maana hii.

3.5 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia uchanganuzi wa semi zilizotumika katika mahubiri na kuleta kupanuka, kukisia na kubanika kwa maana. Imebainika kuwa wahubiri waliorekodiwa walitumia semi nyingi zilizopanuka kimaana, chache zililetu maana ya kukisia na chache kabisa zilibanika kimaana. Semi hizi zilitumika katika viwango tofauti na wahubiri hao tofauti.

SURA YA NNE HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

4.0 Hitimisho

Katika utafiti tuliongozwa na haipothesia hizi;

1. Wahubiri wa kidinihutumia baadhi ya semi zenyе maana ya kiisimu ni tofauti na maana ya kimkutadha.
2. Muktadha wa matumizi ya baadhi ya semi katika matini ya kidini Kiswahili ya kipentekoste huathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu.
3. Matumizi baadhi ya semi katika matini ya kidini kipragmatiki yana umuhimu.

Katika utafiti huu tulikusanya data kutoka nyanjani. Data hii tuliirekodi kutoka vituo vya televisheni vitatu ambavyo vilipeperusha mahubirikatika lugha ya kiswahili. Hii ilituwezesha kupata data inayofaa kulingana na utafiti wetu. Hata hivyo kulikuwa na wingi wa kuchanganya msimbo ambapo wahubiri wengi walichanganya lugha ya Kiswahili na Kingereza lakini haikutuzuia. Tulirekodi data kutoka vituo vya KBC, SAYARE na MBCI ambapo tulirekodi vipindi sita kutoka kwa wahubiri watano.

Kwenye utafiti huu tuliongozwa na malengo matatu. Kwanza tulitabainisha semi zenyе maana ya kiisimu ni tofauti na maana ya kimktadha zinazojitokeza katika mahubiri ya kiswahili ya kidini. Pili tulichunguza jinsi muktadha matumizi baadhi ya semi katika mahubiri ya kiswahili ya kidni unavyoathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu na kisha kutambua umuhimu wa matumizi ya baadhi ya semi hizi kipragmatiki. Kwa ujumla utafiti huu uliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksikaambayo inachunguza jinsi maana ya neno kiisimu inabadilishwa katika matumizi na kusababisha kubanika, kupanuka na kukisia kwa maana.

Katika sura ya pili tulishughulikia dhana ya lugha kwa ujumla na jinsi inavyohusiana na mawasiliano, muktadha, mahubiri kanisani na dini. Tulizungumza kuhusu dhana ya sajili kwa ujumla na kuangazia sifa zinazobainisha sajili kwa ujumla. Baadaye tuliangazia sajili ya kidini

ambapo tumejikita katika huu utafiti na kuzungumza kuhusu sifa za sajili hii kulingana na michango mbalimbali ya wanaisimu na wataalamu wa isimujamii.

Kwenye sura ya tatu tulichanganua semi zilizotumika katika mahubiri kwa misingi ya nadharia ya pragmatiki leksika. Kutokana na utafiti huu tuligundua kuwa baadhi ya semi katika mahubiri tuliyorodi zilizua maana ya kipragmatiki. Matumizi ya semi hizi hayakuwa na utaratibu unaofanana kutoka kwa mhubiri mmoja na mwingine bali zilitokana na ubunifu wa kibinagsi. Wahubiri hawa walitumia semi hizi kwa viwango tofauti kwa sababu kuna wale waliotumia semi nyingi na wengine chache na kwa njia zinazotofautiana. Kutokana na utafiti ilibainika wazi kuwa semi nyingi zilizotumiwa zilipanuka kimaana chache zilileta maana ya kukisia na si wahubiri wote waliotumia semi zilizoleta maana hii.

Katika sura ya nne tulifanya uchanganuzi wa semi zilizobanika kimaana. Kutokana utafiti huu semi hizi zenye kubanika kimaana zilijitokeza kwa uchache sana. Hata hivyo kuna baadhi ya wahubiri ambao hawakutumia aina hii ya semi kabisa katika mahubiri yao. Wale waliozitumia nao walitumia kwa uchache kabisa.

Katika utafiti huu nadharia ya pragmatiki leksika ilinuiwa kutusaidia kueleza mabadiliko tofauti yaliyotokea katika baadhi ya semi wakati wa ufasiri wa ujumbe katika akili ya msikilizaji. Utafiti huu umeonyesha kuwa nadharia ya pragmatiki leksika inaweza kutumika katika uchanganuzi wa semi hizi kikamilifu. Katika uchanganuzi wa semi hizi nyingi zilipanuka kimaana chache zilitokea katika kukisia kwa kimaana na chache kabisa katika kubanika kimaana.

Kwa ujumla imedhihirika kuwa malengo makuu ya utafiti huu yametimilika. Kwanza, tuliweza kubainisha semi katika mahubiri ya kidi zenye maana ya kiisimu ni tofauti na maana ya kimuktadha ambazo zilitumika katika viwango tofauti na wahubiri tofauti. Vilevile imeweza kubainika wazi kuwa muktadha wa matumizi wa baadhi ya semi mahubiri ya kidini ya Kiswahili yanaathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu. Kutokana semi nyingi zilizotumika maana ya kiisimu ilitofautiana na maana ya kimuktadha. Kisha tumeweza kutambua umuhimu wa matumizi ya semihizi kipragmatiki katika mahubiri ya kidini tuliyorekodi.

4.1 Maoni na mapendelekezo

Utafiti huu ulijifunga katika semi kwa ujumla lakini kuna tamathaliza ambazo zinaweza kutafitiwa katika mahubiri ya kidini kama kubadilisha msimbo, nahau, methali na tashibihi. Vilevile utafiti huu uliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika ambayo ni kati ya nadharia nyingi zinazoweza kutumika katika uchambuzi. Pia imejitokeza kuwa kiwango cha masomo cha wahubiri huathiri jinsi wanavyotumia lugha katika mahubiri yao. Kwa hivyo, swala hili linaweza kuchunguzwa pia katika tafiti za baadaye.

MAREJELEO

- Blutner, R. (2001), *Pragmatics and the Lexicon*, Humboldt University Berlin, Germany.
- Blutner, R. (2011) *Some Perspectives on Lexical Pragmatics*, Pragmatics Reader: Routledge, London.
- Buliba na wenzake (2006), *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Crystal, D. (1969), *Language and Religion*, 20th Century Catholicism, New York, Hawthorn Books, USA.
- Ugwueye, E. na Ohaeto, N.E., (2012), *Religious Language: Problems and Meaning*, Uznik Journal of Arts and Humanitis, Vol 12, No. 1 (2011).
- Hillis, D.P. (1997), *Preaching and Communication*, The Army Chaplaincy Summer Fall.
- Hudson, R.A. (1980), *Sociolinguistics*, Cambridge University Press.
- Indede, F. (2007), “Lugha ya Kitamathali katika Mahubiri ya Dini ya Kikristu” Unpublished PhD thesis – Maseno University, Kenya.
- Ipara, I.O. na Maina G (2008), *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*, Oxford University Press, Kenya.
- Iribewangi na Mukhwana (2011), *Isimujamii*, Nairobi Focus Publishers, Kenya.
- Kean, W. (1997), *Religious Language*, University of Pennsylvania, Philadelphia, USA.
- King’ei, G.K. (1992), *Advanced Language Skills in Kiswahili*, University of Nairobi, Kenya.
- Kenya Advisor (2015), *Churches in Kenya: An Overview*, accessed on 02/05/2015

Kiyovu, J.B. (1987), *Introduction of the Study of Language and Linguiistics*, University of Nairobi, Kenya.

Leech, G. (1981 [1974]) *Semantics: The Study of Meaning*, 2nd edn. Harmondsworth: Penguin.

Lawless, E, J. (1988), *The Special Language of Pentecostalizm*, University press of Kentucky, USA.

Mathooko (2007), *Isimujamii: Misingi na Nadharia*, Njivua Books, Nairobi, Kenya.

Mukhwana, A. (1990), “Siasa na uimarikaji wa Kiswahili Kenya”, Unpublished MA Thesis, University of Nairobi, Kenya.

Mutiso, K. (1996), “Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry Kasida ya Burudai” unpublished MA thesis, Nairobi University, Kenya.

Nganje, D. (2008), *Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu*, Jomo Kenyatta Foundation, Kenya.

Nthamburi, Z. (2015), *The Beginning and Development of Christianity in Kenya: A Survey*, Dictionary of African Christian Biography accessed from <http://www.dacb.org/history/beginning%20and%20development%20of%20christianity%20in%20kenya.html> on 02/05/2015.

Nthenya, E.M. (2012), “Communication Strategies by Interpretors from Selected Pentecostal Churches in Machakos town Kenya”, unpublished MA thesis, Maseno University, Kenya.

Okombo, L.P.L. (2011), “Sitiari, Taashira na Tashbiha katika Uwasilishaji wa Dhamira katika Utensi wa Tambuka: Uhakiki wa Kimtindo”, Unpublished M.A. Thesis, University of Nairobi, Kenya.

Okuku, W.M, (2010), “Uchanganuzi wa Kiisumu wa Baadhi ya Matini za Kiswahili Mtazamo wa Pragmatiki Leksika”, unpublished MA thesis, University of Nairobi, Kenya.

Rahimi, A. (2012), “Language and Religion; Linguistic Religion or Religious Language”, Unpublished M.A. thesis, TEFL, University of Kashan, Iran.

Stockwell (2002), *Sociolinguistics*, Routledge, London.

Ugot, M. I. (2013), *Language and Communication in the Pentecostal Church of Nigeria: The Calabar Axis*, Theory and practice in language vol III No 1 Academy publishers, Finland.

Wamitila, K.W. (2008), *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Vide Muwa publishers, Kenya.

Wangui, Z.N. (2010), “Manifestation of Stereotype through Gikuyu Figurative Language: a Lexical Pragmatic Perspective”, unpublished MA thesis, University of Nairobi, Kenya.

Waweru, T. (2012), “Ubabilishaji Misimbo kakita Kanisha la Katoliki”, Unpublished MA thesis, University of Nairobi, Kenya.

Wilson, D. (2003), *Relevance and Lexical Pragmatics*, Katika Italian Journal of Linguistics, Italy.

Wilson, D. na Cartson, R. (2007), *A Unitary Approach to Lexical Pragmatics: Relevance, Inference and ad hoc Concepts*.

VIAMBATISHO

Kituo: KBC Mhubiri: James Ng'ang'a

Tarehe: 06/06/2015

Wakati: 8:15 Asubuhi

Tunawakaribisha katika kipindi hiki cha neno litakuweka huru kutoka hapa neno evangelism centre makutano ya barabara ya uhuru highway na Haile Selassie. Ibaada zetu ni kama unavyoona hapo kwa runinga yako, na tunafanya hiyo mikutano kwa sababu yako. Wewe ambaye unahitaji kiroho, una hitaji ambalo liko juu ya mawazo yako na juu ya daktari na juu ya fedha zako. Aliyebaki sasa ni Mungu peke yake. That's why tutakuwa hapa jumanne na alhamisi. Kukurejesha tena katika anga. Ukija, uje mapema, kwa sababu tunaanza ibaada hizi saa nne kwa sababu ya msongamano wa magari, tuweze nasi kurudi nyumbani. Kumbuka ibaada zetu za asubuhi zinaanza mapema. Very early in the morning Tuesday, Wednesday and Thursday. Friday tunakuja hapa kwa maombi. Na Bwana atakubariki.

Isaiah 58 and number 13, the Lord says, If you treat your servant as a sacred and don't pursue your own interest on that day, if you value my holy day and honor it without travelling, working on that day, then you'll find the joy that comes from serving me.

Kuna vitu vinapatikana katika kumwabudu Mungu. Anasema siku hii mukiitunza, iwe ni siku ya ushirika, iwe ni siku ya fellowship. Musipunje nguvu za madhabahu. Musipunje masaa ya mkutano. Musiende kinyume na matakwa ya mkutano. Musiende kinyume na ibaada. Basi na nyinyi mutapata raha inayotokana na kumtumikia Bwana. Naye anasema hapo chini kwamba, 'Nitafanya ulimwengu ukuheshimu'. 'I will make the nations and the kings to honor you'. 'Nitasababisha', tafsiri ya hiyo ni kwamba God is coming to bless you. He is coming to bless you. He is coming to make the nations honor you. Wale mumezungukwa na maadui, wale mumezungukwa na watu wanaowatafuna kama big-G, wacha waendelee kuongea, maana ni hawa hawa, hawa hawa ndio Mungu atawatumia kusema alikuwa haoni sasa anaona. Alikuwa haongei sasa anaongea. Alikuwa amekonda sasa amenona. Alikuwa hakuolewa sasa ameo. Alikuwa hajaoleta, ameolewa sasa.. Laana yao itawarejelea Wawa hawa ambao walikuwa

wanakuambia hauwezi, upanga wa Goliathi ndio utakaomkata kichwa chake wao. Matusi yao itawarejelea wao. Walipokuona duni watakuwa duni wao. Maana Bwana akianza kukuinua, hakuna binadamu wala pepo anayeweza kumshawishi awache kukuinua. Atakuinua kwa sababu yeze ni Mungu. Atakuinua kwa sababu ni mpango wake. Anasema nilikupenda.

Ninajua umesikia maneno mengi. Na kwa sababu ulitilia maanani, ikazaliwa kwa anga yako. Kwa sababu alikuelezea hivyo, alikuelezea hautafaulu. Na kweli kuanzia siku hiyo, ukaanza kuona mambo yameenda chini. Sitaki kujua ulikula nini. Sitaki kujua hiyo nguo alikupatia ilikuwa na nini. Sitaki kujua hizo pesa. One thing I know, there is power in the name of the lord Jesus Christ. Kitu kimoja nakuomba tu, wale mumeota, you have the power to change that. Wale mumeambiwa maneno mengi, you have the power to change that. Tukianza kumwabudu huyu baba wetu wa binguni, wale wamesema wewe ni masikini, jibatize, because the Lord breathed. Bwana akapulizia. Akaregeshea mitume kile ambacho watu wa kwanza hawakuwa nacho.

Wale watu wa kwanza hawakuweza kuamrisha mapepo. Hawakuweza kuwaamrisha waganga na wachawi. Lakini the new power that God is giving you today, you have the power to control them. You have the kingly spirit. Ile roho uko nayo, ni zaidi yay a hawa unaona wakiongoza Kenya. Hawa unaona wakiongoza ulimwengu. Kile ambacho kiko ndani yako, I wish baba yangu anaweza kukubali akutoe leo kidogo, akuonyeshe. Zile uniform uko nazo, zile magwada za kijeshi ya binguni. I Jehova anaweza kuwafungueni macho, ukaona malaika jinsi wamewashughulikia. Ukanoa jinsi wanakimbia kufungua milango. Kama vile unaona president akipita. Magari yote itasimama. Aidha ni ya mgonjwa, aidha ni ya wazimamoto, haiwezi kukutana na ya president. Hiyo moto itaendelea kuchomeka. Huyo mgonjwa nine nine itaendelea kulia hapo. I wish bwana akufungue kidogo. Unaenda mbali. I wish baba akuonyeshe kule ambako unaenda. Nikisikia magari zikiguruma, zikianza kuondoka.

Niruhusu nikuambie tu, yule alikuambia hautaweza, mimi ninakuambia, uliweza zamani. Ulishinda zamani, si ati utashinda. Ulishinda. Vita yoyote ambayo baba yangu ataiwachilia kwako kuanzia leo, ukifika jioni uone zimechacha, weka kikombe ya chai, ukunywe muambie baba ahsante kwa sababu umenichagua. I didn't know I would reach this level in Nairobi. Ambia jirani yako I am chosen by God. Ambia jirani yako mwingine mwingine, mwambie Mungu ananipenda. Mwambie mimi ni rafiki ya Mungu. Na jinsi ambavyo utaona magumu yakikukujia, hivyo ndivyo upendo wa Mungu ulio mkubwa juu yako. Na inavyozidi kuongezeka. Shetani

anataka kukuonyesha Mungu hakupendi. Wewe ni mtu mkubwa. Wi mundu munene. Wewe ni mtu mkubwa. Magazeti itakupiga, redio zitaongea, mtaa mzima itaongea na watakuacha umesimama. Jinsi wanavyoongea kinyume chako ndivyo bwana anazidi kukuinua. Watapigana na wewe, na hawatakuweza. Jiachilie sasa, toka kwenye haya maroho uliambiwa na uanze kujiambia, uanze kusema I am a winner, I am going to win this battle. I am going to conquer. Ninaenda kupeperusha bendera katika familia, kama vile Daudi alifanya. I am going to sing many songs.

Exodus 32 and number 30 all the way to number 34. The next day Moses said to the people, you have committed a terrible sin, and now I will again go up the mountain, perhaps I will obtain forgiveness for your sins. Moses then returned to the Lord and said, these people have committed a terrible sin. They have made a god out of gold and worshipped it. Please forgive their sin. But if you won't, then remove my name from the book in which you have written the names of your people.

Musa alipokuja, alikuta watu wamekwisha wacha kuabudu Mungu, na wanaabudu vinyago. Naye Musa akasema, wacha niende kwa Mungu, labda naweza kupata... perhaps I will obtain the forgiveness. Then Moses went back to the lord to the mountain. Musa akaenda akaambia Mungu, kama hautasamehe watu hawa, ondoa jina langu kwenye kitabu kile cha uzima. Naye Mungu akamwambia Musa, ni wale walionikosea ndio nitakaoondoa wao kwa kitabu kile cha uzima. Lakini sasa ondoka upeleke watu hawa kwenye yale mashamba niliwaahidia. Na malaika wangu ataenda pamoja na wewe.

Kazi hii ninafanya siwezi kufanya bila msaada utokao juu mbinguni kwa Mungu. Ile kazi ambayo tunaenda sasa safari hiyo, hauwezekani bila usaidizi wa kiroho. Ninawaomba tu wapendwa wenzangu, kama unaona mambo yamekuwa magumu katika macho yenu ya kuona, just go in the spirit world. If you want to know about things will happen, if you want to know your status, if you want to know your situation, just go in prayers. And when Paul was praying in Jerusalem, the Lord appeared to him and said, don't waste your time here, because these people will not accept. Somewhere in the acts, when Paul was still praying, kisha akaona maono, Yesu akimwambia, sasa hapa usiondoke kwa sababu, niko na watu wengi watakaokusikiliza.

Wakati mambo yamekuwa magumu kwako katika ulimwengu wa kimwili, basi yaangalie katika ulimwengu wa kiroho. Mungu ameniambia muache kufanya kesi kwa mwili, mufanye kesi katika kiroho. Na baba amesema, mfalme wa wafalme, Mungu aishiye milele, amesema, musikubali kesi yako ifanyiwe uamuzi na shetani. You don't belong to the devil. You belong to God, let your case be done in the house of the Lord. Somebody say Amen.

Na Mungu akamwambia Musa, sitaondoa jina lako, lakini jina ya hawa wamenikosea. Kuna mtu jina lako limeondolewa. Na unajua likiondolewa hapo ndipo al-shabab wanapitia. Unajua likiondolewa na ukose kufanya bidii lirezeshwe, hapo ndipo sasa utajikuta kwa mpango wa accident. Hawa watu naona shetani akimaliza kwa accident moja. Huwa amewakusanya in the spirit world. Amewaweka kwa ile gari anajua anakwenda kuibomoa. Akienda pale aone majina yao hayako, anakuwa na uwezo wa kuwaua kabla hawajarudi tena.

Inamisha uso wako. Bow down your head.

Kituo: SAYARE Mhubiri: Eli Rop

Tarehe: 05/06/2015

Wakati: 9:04 Usiku

Kwa kweli, tarajio kubwa la kanisa, hili ni jambo la muhimu sana ambalo kila mmoja wetu tusingelipenda kukosa, ni kunyakuliwa Yesu atakaporudi. Unaweza kukosa mambo mengine mengi tuliyuo nayo hapa duniani, kwa mfano, wengi, tumeomba Mungu kwa ajili ya miujiza, muujiza wa kazi, muujiza wa pesa, muujiza wa kuo, muujiza wa kuolewa, muujiza wa nyumba, miujiza kadhalika na kadhalika. Na labda ungesikia kwamba umengojea sana. Na huenda ikawa utangojea siku zote za maisha yako. Na huenda Mungu asikujibu katika neno hilo. Lakini nakusihii sana katika jina la Yesu Kristo, usikose wakati ule, parapanda itakapolia.

Mfululizo wa mafundisho niliyoyatilia mkazo sana ambayo kwa upande mwingi kanisa ni kama tulianza kusahau. Kwa sababu tulianza kuona kanisa kama ilivyo tukaangalia upande mmoja. Si upande mbaya, upande wa kubarikiwa, upande wa kuomba miujiza na ishara. Ni vizuri. Ukaanza

kuona ni kama tulianza kuelekea zaidi upande huo, kuliko kuangalia shabaha kamili ya ndani. Tukasahau ya kwamba, hata muujiza ilivyoje inaweza kutendeka na zinaweza kukuacha. Hata Mungu akikupatia bilioni mia moja leo, ni pesa ambazo zitabaki dunia. Hata ukijenga magorofa, itaisha kwa sababu parapanda itakapolia, utanyakuliwa. Hata ukipata nafasi ya kupona, na ninataka upone katika jina la Yesu. Lakini hata bado ukipona, nilieleza katika kipindi kingine ya kwamba, hata Lazaro alifufuka kutoka kwa wafu, lakini leo hii, Lazaro hayuko hai. Bado alirudi kulala tena.

Lakini muujiza mmoja ambao kila mmoja wetu ni lazima tupambanue, lazima tupiganie, lazima tutilie mkazo, ni muujiza huu wa kunyakuliwa, Yesu atakaporudi. Na muujiza huu utatendeka kwa wale ambao walitii amri Yesu Kristo alitoka kwa wanafunzi kwamba enendeni ulimwenguni kote mukawafanye watu kuwa wanafunzi.

Tunafundisha alama nne za muhimu za kuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo. Tukaangalia kwamba alama ya kwanza ni mtu kuzaliwa mara ya pili. Kwa kutubu dhambi zake, kwa kugeuka. Tukaangalia kuwa ya pili, mtu aliye mwanafunzi wa Yesu Kristo anatoa uhai wake anatoa maisha yake kwa ajili ya Yesu Kristo. Tukaona alama ya tatu ya mwanafunzi wa Yesu ana maisha ya kujitolea. Anatoa ushuhuda. Anafanya kazi ya bwana, kwa kujitolea, si kwa kulazimishwa. Na tukaona alama ya nne, mwanafunzi wa Yesu Kristo anatoa mali zake kwa ajili ya kazi ya injili, bila kulazimishwa. Bila kufanya biashara na Mungu.

Leo hii, ningependa kujenga zaidi tena, kwa sababu tutaendelea na masomo hayo ya shabaha ya injili ya Yesu Kristo kwa kipindi kile roho mtakatifu atakavyotuwezesha.

Tukirudi katika nambari ile ya kwanza, mtu anapozaliwa mara ya pili, unaposamehewa dhambi zako, bibilia inasema kwamba, imekuwa basi, mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipywa, ya kale yanapita. Tazama yote yanakuwa mapya. Paulo akatilia mkazo zaidi akifundisha. Akasema basi kama umezaliwa mara ya pili, kwa kumwamini Yesu Kristo. Katika wakolosai tatu kuanzia aya ya tano, akasema, basi, ueni, angamizeni, malizeni tabia yenu ya zamani iliyo katika miili yenu. Akaanzia jambi usherati, uchafu, akaendela, na akaendela, na akaendelea mpaka akamalizia ibaada ya sanamu. Kuua, kumaliza. Halafu katika mstari wa sita, akasema kwamba, maana hasira ya Mungu inakuja juu ya wale watu wasiotii. Ukifikiri mambo haya yote,

ambayo, hata ndani yake yamejaa tamaa, ndani yake imejaa mazungumzo yasiyo na maana, ndani yake imejaa uzinzi, na uchafu.

Mambo haya ambayo watu siku hizi wamekuja nayo katika nyumba ya Mungu. Si wote, kuna wale ambaao wamejaa utakatifu. Lakini leo hii kwa sababu tunakutwa na chamgamoto katika kanisa la bwaba, hasa manabii wengi wa uongo, ambaao wanataka kuzoa wanafunzi kwa ajili ya faida ya pesa zao. Wamefanya injili kuwa too cheap, too easy. Kwa hivyo ukitaka kuhubiri utakatifu na usafi, wale wanaokuja na kubuni njia rahisi wanazoa wanafunzi.

Na unakuta kwamba mwanadamu hawezi kutenda ukweli. Mwanadamu mara nyingi anapenda kudanganywa. Ukihubiri injili iliyojaa utakatifu, na usafi, na ukweli, watu watakuacha. Tukirudi katika desturi ya makanisa ya zamani, ambapo mtu alipokutwa na dhambi, alitengwa, alisimamishwa, alitajwa mbele ya kanisa. Leo hii, unasimama na kumtenga mtu ambaye ametenda dhambi, unakuta mhubiri mwingine ako kando hapo tayari kumpokea na kumwambia kwamba watu kama wewe hawatakikani huko. Baadaye inafanya kwamba habari hiyo inafanya kanisa ku-compromise. Kukengeuka. Kusema kwamba sasa tukitenga watu, watu wengine wako tayari kuwapokea. Ukijaribu kusema kwamba huu ndio utakatifu, watu wengine wako tayari kuwachota. So unakuta kwamba, hata wale ambaao wangehubiri ukweli, wameanza kuogopa kuhubiri ukweli. Na hapo ndipo tumeanza kukubali mambo yasiyo safi katika nyumba ya Mungu. Lakini tunasahau ya kwamba, tunaweza kuwapata watu katika makanisa yetu. Tunaweza kuwajaza watu elfu elfu. Tunaweza kuwajaza watu mpaka unakuta kwa kanisa watu elfu mia tatu, watu milioni moja. Tunaweza kuwajaza. Lakini ujue kwamba watu wasio safi, hawataingia mbinguni. Kwa hivyo, kama ni mhubiri wa kweli, tunayejali kuwa Yesu atakuja, tunahitaji kutengeneza quality ya watu watakaoingia mbinguni. Lazima tuangalie vizuri.

Paulo anasema katika Wakolosai tatu msitari wa sita kwamba, wale wanaotenda mambo kama hayo ambayo ametaja katika Wakolosai tatu aya ya ya tano, hasira ya Mungu, hasira ya Mungu. Wakati mwingine tunasema tunaishi wakati wa neema, ni sawa, sikatai. Lakini katika agano jipya hili hili tu, Paulo anasema wale wasioishi kwa namna inayompendeza Mungu, hasira ya Mungu itawaangukia wana wasiotii. Wale wanaokengeuka. Tunajaribu kufanya neema ya Mungu kuwa so easy. Na hii ndiyo imefanya mpaka kanisa inachanganyikiwa. Naomba kwamba unanisikiliza kwa makini, neema ya Mungu iko. Na yule anayesikia na kutubu, na kuacha.

Na hapo ndipo bwana anatuambia katika msitari wa... mbele hapo ya kwamba, utoe utu wa zamani, tuvye yule mtu wa kale. Hebu nisiadie kidogo niangalie maandiko matakatifu. Katika Waefeso nne, kuanzia msitari wa ishirini na mbili. Anasema kwamba, itoeni namna ya zamani, vua utu wa kale. Kwa hivyo, kuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo baada ya kuokoka na kuzaliwa mara ya pili, vua utu wa kale. Mara ingine nimefikiri nakutaja katika mafundisho ya kwamba adui ya mkristo mara nyingine, ndiyo tunajua kwamba adui kama vile bibilia imetuambia katika Petro ya kwamba yule ibilisi anazunguka, mshitaki wetu kama simba angurumaye anatafuta anayemmeza. Ndiyo hii ni adui wetu, lakini mahali gani anapata field? Mahali gani anapata kiwanja cha kutupiga? Ni katika utu wetu. Hasa utu wa kale.

Ukishaokoka na kumwamini Yesu Kristo, na bado unataka kuvalaa ule utu wa kale, inakuwa ngumu sana. Tumekuja kwa nyumba ya Mungu, tumeokoka. Kusimama na kusema kwamba nimeokoka ni sawa. Kuimba, kushika kitabu cha tenzi cha rohoni na kuimba si ni kama kuimba nyimbo zingine ambazo hata hazikuhusu wewe. Haloo? Kuna zile nyimbo za dunia ambazo watu waliimba ambayo haikuwahusu. Mtu anaimba juu ya mpenzi wake ambaye sijui alifanya nini. Unasikia wimbo ambao kwa sababu una rhythm mzuri na ina utamu wa maneno, mtu anaimba, mpenzi wangu eeee, mpenzi wangu eeee, na ahata huyo mpenzi hajakuwa naye hata kwa maisha. Na mpenzi mwingine ni mwanamke anaimba na yule ambaye alikuwa anaimbiwa ni mwanamume. Sasa unasikia ni mchanganyiko. Watu wanaweza kuimba mambo ambayo hata haiwahusu. So unakuta katika nyumba ya Mungu watu wanaweza kuimba wimbo ambao haiwahusu. ‘Ni siku kuu, siku ile, ya kumkiri mwokozi...’ na hajakiri mwokozi. Bado ana utu wa kale, bado ana tabia ile. Halafu anasema, ‘Mungu anajua tu siku moja....’. Mungu hawezikujua kama amesema uvuliwe utu wa kale. Kwa hivyo adui mmoja mkubwa wetu sisi, hata si ibilisi. Ni mwili wako mwenyewe. Ni adui mkubwa.

Katika somo iliyotangulia tulisema kwamba aliyemwamini Yesu Kristo katika maisha ya kujitoa kwa ajili ya Yesu unasulubisha mwili. Bibilia inasema vizuri ya kwamba, anayetaka kunifuata ajikane mwenyewe. Kuona mambo ya Yesu kuwa ya faida zaidi kuliko mimi mwenyewe. Kuchukua mambo ya Yesu kuwa ya faida zaidi kuliko yangu mimi mwenyewe.

Hapo ndipo moja ya mitihani kubwa ya ukristo. Kama tungejua mtihani huu mkubwa, katika taifa la Kenya mabapo watu asilimia themanini wanaenda makanisani, tusingesikia mambo ya ufisadi. Mahali ambapo asilimia themanini ni watu ambao wamepata jina la kikristo kwa

kubatizwa. Kama kweli jambo hili la desturi za kanisa ingekuwa njia, utu wa kale ungekuwa umevuliwa, usingekuta watu wanaouana. Usingekuta... usingekuta watu wanaotendea wenzao ujeuri. Usingekuta. Usingekuta mafaragano, malumbano, masengenyo, madharau tunayoshuhudia leo katika kanisa la bwana. Mionganis mwa malumbano na mashindano hata si mionganis mwa washiriki tu. Si wale wakristo waliookoka jana. Hapana. Inawahu su wakristo wa zamani. Inawahu su wazee wa kanisa waliowekewa mkono. Inahu su maaskofu walio na majina ya heshima. Walio viongozi wa madhehebu makubwa makubwa. Lakini ndani yao, kumejaa ufisadi. Kumejaa chuki. Kumejaa madharau. Kumejaa mauaji bunduki na risasi kumtwanga. Ukimdhara, ukimtukana, ukimchukia, tayari mbinguni inasema umeua. . Kwa sababu bibilia inasema kwamba, iwapo unamchukia mwenzako, wewe ni muuaji. Hauna haja ya kushika

Nasikia sauti... wengine wakisema, kama ni namna hiyo, heri, itakuwa ngumu kuingia mbinguni. Sio hivyo! Si bibilia inasema kwamba njia ile ya kuenda mbinguni, barabara ni nyembaba sana na wachache wanaipata. It means kuna wale watakaoipata. Ni ukweli kwa wale wanaosikia mafundisho haya ambayo ninafundisha leo ambayo yananenwa na roho mtakatifu.

Bibilia inasema ya kwamba, ivueni utu wa kale. Put off the old man. Mtu wa kale, yule ambaye ulikuwa naye. Mwingine kabla ya kuokoka na kumwamini Yesu, hungemuonyesha kidole namna hii... angekiuma. Anasema kwamba, we, kabla ya kuokoka, hungeonyesha kidole. Tungekutana. Leo hii baada ya kuokoka, unaonyeshwa kidole mara kumi, hata unafanywa namba hii... bado unasema Mungu akubariki. Kama hauwezi sema Mungu akubariki, ujiulize kama umetoa utu wa kale. Niliambiwa na mtu mwingine kwamba kuna watu amba ungetaka kujua kama wameokoka kweli angusha shilingi. Kama hatainuka... kama shilingi ikianguka ndingli asipoinuka, utajua amekufa kweli, kwa sababu, akisikia sauti ya shilingi, hata kama atakuwa amelala, atainuka tu.

Hiyo ndiyo tunaita utu wa kale. Utu wa kale wa makabila mengine wamejaa kiburi. Utu wa kale wa mahali pengine, yaani usipomsifu, wewe, usipomtambua, wewe! Ni taabu. Utu wa kale. Mtu mwingine akakasirika ati ameitwa ng'ombe. Mpaka akafanya vita ati kwa sababu aliitwa ng'ombe. Nikajiuliza, kwani ukiitwa ng'ombe umekuwa ng'ombe? Si ni yule ambaye anakuita ng'ombe ndiye ana taabu kwa sababu wewe si ng'ombe. Na hutakuwa ng'ombe. Hata akisimama juu ya mlima na kusema ng'ombe mara mia moja, hutakuwa ng'ombe. Kwa hivyo, unakasirikia nini? Mpaka umetwanga mtu mpaka jino limeenda mpaka macho... jicho limekufa... la mtu.

Halafu ukiulizwa kwa nini? Ati aliniita ng'ombe. Ati alinitukana. Hata nikikuita ng'ombe, hautakuwa ng'ombe! Ni kitu gani linakufanya unatwanga mtu kwa sababu amekuita ng'ombe? Ni utu wa kale ambao haujavua. Ukivua utu wa kale, hata ukiniita ng'ombe, I have no problem. Kwa sababu mimi si ng'ombe. Na sitakuwa ng'ombe. Na sitakuwa ng'ombe. Mimi ni mtu, mwanadamu, Eli Rop. So, ukiniita kile ambacho unaniita, its your problem. Kwangu mimi si problem. Ni kwako wewe unayeniona ukifikiri mimi ni ng'ombe. Wewe ndiwe una taabu. Kwa sababu hujaniona vizuri, ukaniona ukafikiri mimi ni ng'ombe, lakini mimi ni binadamu. Kwa sababu nimevua ule utu wa kale. Hainijalishi! Hainijalishi! Ninachojali mimi mwenyewe ni kuishi katika maadili. Kwa hivyo nikivua utu wa kale, hata ukinichokora, hata ukinisema, hata ukinionyesha kidole, hata ukinionyesha madharau, hata ukitema mate ndi, chini kwa ajili yangu, hainijalishi. Kwa sababu niliuvua utu wa kale ambao ungetema mate, ungenidai nilipishe kisasi. Kwa hivyo sitalipisha kisasi!

Mtu kuvua utu wa kale. Huyu mtu wa kale anavuliwa wapi? Katika Waefeso ule nne, msitari wa ishirini na tatu Paulo anasema kwamba, mubadilishe mawazo yenu. Na hapo ndipo mkristo ye yote unadai kabisa. Una haja ya kubadilisha nia na uwe na mtazamo wa Yesu Kristo katika maisha yako. Hiyo wakristo wengi wana mtazamo kama mtazamo wa dunia. Wanafanya biashara kama vile dunia inavyofanya. Wanafanya ulaghai kama vile dunia inavyofanya ulaghai. Pesa nyingi ambazo zinapatikana katika nyumba ya Mungu hazipatikani kwa haki. Ni kwa njia ya ulaghai kama vile dunia inavyofanya ulaghai. Ni kwa pata potea. Unaambia watu jambo hili, ukimaanisha hili. Unachangisha pesa kwa ajili ya jambo hili, lakini shabaha ya hizo pesa ni hili. Unaanzisha mradi ukisema kwamba unajali masikini, na kumbe masikini namba moja ni yule ambaye anachanga hizo pesa. Kwa hivyo, kuna ulaghai, kwa sababu, mawazo tulio nayo mara nyingine, tunawaza kama vile dunia inavyowaza. Kama tunajali kurudi kwa Yesu Kristo, kama tunajali, sina mtu wa kale. Kwa kubadilisha nia. Kwa kubadilisha mtazamo. kunyakuliwa kwa kanisa, kama tunajali kweli kwamba siku ile parapanda itakapolia, niwe mionganoni mwa wale watakaonyakuliwa

Mtazamo unababilishwa kwa namna gani? Mtazamo unababilishwa kwa kusikia neno la Mungu. Na neno la kweli, si neno la kudanganya. Kila mmoja wetu, umepewa hisia na Mungu. Hata unapohubiri, unapotangaza habari njema ya Yesu, Kristo, ninapoeleza jambo hili la uzima wa Yesu Kristo, utajua kutofautisha. Mimi najua wengine wanatafuta TV, wanatafuta vipindi vyaa

watu ambao wanasema, ukifanya hivi, ukifinya button hii, hii itatendeka kwako. Wanafanya vitu kama hivyo. Na hawataki kubadilisha nia. Wanataka kutendewa badala ya kutenda. Wanataka kubarikiwa badala ya kubariki. Wanataka mwingine awaendee binguni badala ya hao wenyewe kuenda. Na hapa ndipo taabu. Lakini ukibadilisha nia, kutafuta namna, utasoma maandiko matakatifu na kuomba roho mtakatifu njia gani ni njia ya kweli na huwezi kupotea.

Bibilia inasema katika barabara hii ya watakatifu, watu hawapotei hata kama ni wajinga. Which means kuna roho wa bwana anaongoza wale ambao ni watakatifu walio na nia ya kuenda mbinguni kweli hawapotei katika njia hii. Hawakosei. Kwa hivyo ukitaka kweli kutokudanganyika, hata hapo Paulo ametuambia katika msitari wa ishirini nan ne ya kwamba mionganoni mwa utu wa kale, hasa katika ishirini na tano, akasema kwamba ni uongo. Kile kitu kinafanya watu wengi kutotoa mtu wa kale ni katika kudanganyika. Hata na sisi. Hata pamoja na wa kudanganywa na ibilisi, pamoja na kudanganywa na wale manabii wa uongo, udanganyifu wa kweli namba moja ni wewe mwenyewe kujidanganya. Usipokuwa na nia safi katika moyo, unajidanganya. Usipokuwa na nia hii na hamu hii ya kwamba siku moja nataka kuingia katika uzima wa milele, unajiambia kwamba, bwana, siku moja nataka kuingia katika uzima wa milele. Mahali ambapo unatumaini, mahali ambapo kuna kuishi vizuri pamoja na wewe. Ukijiambia hivyo, hapo ndipo unaweza kuwa na hamu ya kubadilisha nia. Hapo ndipo unachunguza maandiko na kusema ni kitu gani kilicho kizuri. Bibilia inasema ya kwamba, tuondoe uongo, tuambiane ukweli.

Katika kipindi hiki cha Yesu yuaja, jinsi gani ninaomba roho wa bwana atupe neema yake tuambiane ukweli. Tuambiane lile neno ambalo siku moja, na hili ndilo hamu yangu, na ombi langu, kwamba mimi mwenyewe nahubiri, nitibu katika namna hiyo, ninavua utu wa kale, tumaini langu tarajio langu, ombi langu, hamu yangu, bidii yangu, juhudii yangu, ili, siku moja parapanda itakapolia, mimi mwenyewe Eli Rop nirithi uzima wa milele.

Maombi yangu ya pili kubwa, ile ambayo siachilii mbali, ni wewe ambaye unanisikiliza kwa kipindi hiki, upate ujumbe kwamba nilikuambia ukweli, ukatoa utu wa kale, ukautoa uongounaodanganywa. Mahali ambao unadanganywa kuwa ukikuja katika ushirika wetu, ooo hii ndiyo kanisa la ukweli, oo ukikuja katika ushirika wetu, sisi ndio wasafi, hakuna kanisa la ukweli isipokuwa mtu mwenyewe, utubu kwa moyo wake na kuondoa utu wa kale kwa kadiri ya

maandiko ya Yesu Kristo. Bibilia inasema vizuri ya kwamba, hapana jina jingine tulilopewa chini ya mbingu itupasayo kuokolewa kwalo.

Najua katika matendo ya mitume nne kumi na mbili, si majina ya madini zetu, si majina ya maaskofu, si majina ya manabii fulani walio hapa duniani, si majina ya watakatifu Fulani waliotutangulia. Hapana. Ukweli ni kwamba, Yesu ndiye njia na kweli, na uzima wa milele.

Mtu haji kwa baba ila kwa Yesu. Yesu mwenyewe alisema mambo hayo. Yohana kumi nan ne msitari wa sita, ‘mimi ndimi njia, ukweli na uzima’. Na inapotafuta kujua ukweli wa maneno ya Yesu Kristo, si kujiounga na dhehebu fulani. Unapotafuta kujua njia ya Yesu Kristo, si njia ya Maombi fulani. Si njia ya fungu la kumi. Si njia ya sadaka. Si njia ya kufunga. Si njia ya mambo hayo yote ambayo watu wamezoa na kuleta. Ni njia njia ya kumwamini Yesu. Na kubadilisha nia yako kwamba Yesu ni yote katika yote. Na kwamba unatii sauti ya roho mtakatifu kwa kubadilisha nia yako. Hapo ndipo unazaliwa mara ya pili. Na roho wa bwana anatia muhuri ya kuwa wewe ni mtoto wa Mungu.

Utakuwa na uhakika wa kuingia mbinguni siku moja. Na hiyo ndiyo ukweli. Hiyo ndiyo ukweli. Madhehebu ni mengi. Sikatai, kuna sababu Mungu aliyaruhusu yawe nyangi. Lakini njia ya kuenda mbinguni ni moja. Manabii ni wengi. Ndiyo. Lakini si wote wanahubiri ukweli. Ukibadilisha nia yako utafute njia ya ukweli.

Ndugu mmoja alisikiliza ujumbe wetu mahali fulani. Alikuwa ni mgonjwa, ugonjwa wa cancer. Alikuwa kwa dini ingine ambayo haimani Yesu Kristo. Sitaki kukuambia ni gani. Akawa mgonjwa. Alikuwa karibu kufa. Alikuwa mgonjwa wa cancer. Alikuwa ameambiwa kwamba atakufa. Alipota kwa hospitali, ya kwamba anangojea kufa, akaingia katika chumba chake na akaona televisheni yetu ya sauti ya rehema. Akapata mhubiri fulani, haikuwa mimi. Alikuwa ndugu mmoja mpPENDWA, ambaye ni mmoja wa wahubiri wetu. Akamsikiliza kwa makini. Akajiambia aliposikiliza huo ujumbe, akasema kwamba, siamini maneno haya ambayo huyu mtu anasema. Hasa kuhusu huyu Yesu ambaye anasema kwamba yu hai. Akasema kwa kiingereza kwamba, lakini, nikiwa kwa bahati, if per chance, Jesus you are alive, if per chance, yaani akasema, ikiwa kwa bahati, Yesu wewe ni hai, uniponye. Na ukiniponya nitakuamini. Ghafla, katika chumba chake, alipata nguvu kama ya stima. Ikomshika ka. Bila mhubiri mwengine ye yote, bila mtu kumwekeea mkono, bila kufanyiwa mambo hayo mengine yote. Alipona papo

hapo. Papo hapo. Papo hapo katika chumba hicho. Aloposema kwamba Yesu, if per chance, wewe ni hai, uniponye.

Wajua kuna namna ambayo unatafuta Mungu ukisema kwamba bwana, mimi niko hapa. Na wewe umechanganyikiwa wahubiri wengi wamekuja hapa. Mara ya wengine wa panda mbegu, mara ya wengine ombo na kugunga, mara ya wengine fanya hivi mpaka umechanganyikiwa mpaka haujui. Nakushauri kitu kimoja unapobadilisha nia yako, mwambie Yesu, nimechanganyikiwa na mambo haya yote, lakini Yesu, mahali popote pale ulipo, naomba unisikilize. Uniokoe, unyoshe mkono wako mimi niko hapa.

Unahitaji Yesu, utashangaa Yesu ataonekana kwako. Hata sitaki kusema kwamba nitakuombea. Mimi ni ndugu kama wewe. Ninakuambia tu ukweli. Lakini Yesu anakusikiliza, anakuona, anakujali. Anakupenda, angependa kukuinua na kukubariki. Kama vile huyu ndugu alisema kuwa siamini mambo ya huyu mhubiri lakini Yesu ikiwa kwa bahati uko, uniguze, na Yesu alimponya cancer. Ni kama miaka mine sasa imepita. Ni jambo la kweli. Hata wewe ukimwambia, pale pale ulipo, Yesu ni wa kweli, yeye ni mwaminifu. Uvue utu wa kale. Kuwa mwanafunzi wa Yesu ni kuvua utu wa kale. Kuvua uongo. Kuvua tabia tulizotoka nazo duniani. Kuvua tabia... tabia... tabia ya ukabila. Bibilia imesema kuwa hapa ukishaingia hakuna myahudi wala myunani, hakuna mwanamke wala mwanamume. Sote ni moja katika Kristo. Ikiwa katika lugha yako, wewe ni mwanasiasa, wewe ni mkristo, wewe ni askofu, ndani yam domo wako bado unanena ukabila, haujavua utu wa kale. Na hii itatuletea taabu, kutokunyakuliwa siku moja, parapanda itakapolia. Umuombe Yesu kwa moyo mkunjufu, atakusikia, atakuokoa.

Kituo: **KBC Mhubiri:** Pius Muiru

Tarehe: **24/05/2015**

Wakati: **7:51 Asubuhi**

Kuna mambo mwanadamu unaweza kuyapitia ya kwamba watu wote watakuambia Mungu amekuacha. Lakini ndani ya moyo wako, unasikia kushawishika, na kushuhudiwa, ya kwamba Mungu hajakuacha. Ni mapito tu kwa muda Fulani, na baadaye Mungu atakubariki.

Sasa tunaangalia kitabu cha Ayubu chapter number 42, na verse number 14 na verse number 15 mahali neno linatuambia ya kwamba alikuwa na wasichana warembo sana. Yaani urembo unatokea nyumbani kwa Ayubu, nyumba ambayo miaka kadhaa iliyopita, kulikuwa hakuna chochote ambacho unaweza ukasema ni kirembo.

Sasa hivi maishani mwako, hakuna urembo wowote. Lakini mimi nimekuja kuprophesy that beauty is just about to strike into your family in the name of Jesus Christ, even the son of the living God. Sasa wasichana watatu wa Ayubu majina yao yamepeanwa. Na katika majina yao, kuna mahubiri tosha. Msichana wa kwanza anaitwa Jemimah. Msichana wa pili anaitwa Keziah. Msichana wa tatu anaitwa Kellen Hapuch.

Msichana wa kwanza ni Jemimah, maana ya jina Jemimah ni day by day. Yaani, kuanzia sasa, anza kuishi maisha yako ukimtzamia bwana day by day. Ya kwamba Mungu aliye kushindania leo ni yeye atakayekushindania kesho. Every day of your life iko mikononi mwa bwana. Hakuna wakati utakosa kuuona urembo wake bwana, uzuri wake bwana ndani ya maisha yako. Ndiyo maana jina Jemimah ni day by day.

Msichana wa pili anaitwa Keziah. Na maana ya jina Keziah ni ile spice inafanana na cinnamon inaitwa cassius. Keziah ni spice. Na Casius spice inafanya chakula iwe ya kutamanika. Na wakati mwingine vitu vya kujirembesha vinawekwa spice harufu iwe nzuri. Hivyo, tunaona ukiwa na Keziah nyumbani maana yake maisha yako yanakuwa spiced upna kuliko ukae maisha ya boredom na stagnation, unakuwa na maisha ambayo yamekuamka, yana furaha, yako na ucheshi.

